

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

BUNGE LA KUMI NA MOJA

MKUTANO WA KWANZA

Kikao cha Kwanza - Tarehe 17 Novemba, 2015

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Naomba tukae.

TANGAZO LA RAIS LA KUITISHA MKUTANO WA BUNGE

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa masharti ya Katiba, Mkutano huu wa Kwanza unaanza kwa Rais kuitisha. Naomba kuchukua nafasi hii kusoma Tangazo la Rais kama ambavyo tumelipokea.

Tangazo la Serikali Na. 513 la tarehe 6 Novemba, 2015. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Sura ya Pili, hati iliyotolewa kwa mujibu wa Ibara ya 90(1). Hati ya Kuitisha Mkutano wa Bunge Jipya.

KWA KUWA, Uchaguzi Mkuu ulifanyika tarehe 25 Oktoba, 2015 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977;

NA KWA KUWA, masharti ya Ibara ndogo ya kwanza ya Ibara ya 90 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, yanamtaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitisha Mkutano wa Bunge Jipya kabla ya kupita siku saba tangu Tume ya Uchaguzi kutangaza matokeo ya Uchaguzi Mkuu;

NA KWA KUWA, matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 25 Oktoba, 2015 yalitangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi tarehe 29 Oktoba, 2015;

HIVYO BASI, mimi John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mamlaka niliyonayo chini ya Ibara ya 90(1) ya

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, naitisha Mkutano wa Bunge Jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ufanyike katika ukumbi wa Bunge uliopo Mjini Dodoma tarehe 17 Novemba, 2015 kuanzia saa tatu asubuhi.

Kwa kuthibitisha, naweka saini yangu na muhuri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Hati hii leo tarehe 5 Novemba, 2015 Dar es Salaam. Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, Rais.

Naomba kuwasilisha Tangazo.

UCHAGUZI WA SPIKA

DKT. THOMAS D. KASHILLILAH - KATIBU WA BUNGE: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 9(7), nachukua nafasi hii ili sasa Mkutano huu wa uchaguzi uweze kuanza. Kwa hiyo, naomba kumtaja Mwenyekiti ambaye atakalia kiti hiki. Namwomba Mheshimiwa Andrew John Chenge ambaye ndiye Mbunge wa muda mrefu zaidi kuliko wengine aweze kukalia kiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chenge, karibu! *(Makofi)*

Hapa (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Mheshimiwa Katibu wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge, kwanza nawashukuru sana kwa imani ambayo mmeonesha kwangu, lakini ni imani ambayo inatokana na utumishi wangu katika Bunge hili tangu mwaka 1993 nilipobahatika kuteuliwa na Rais, Mzee wetu Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mpaka kipindi chake kilipomalizika. *(Makofi)*

Nilibahatika tena kuteuliwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu kwa wadhifa huo huo ambao niliendelea nao mwaka 2000 mpaka 2005. Baada ya pale nilienda kupata ridhaa ya wananchi wa Jimbo la Bariadi Magharibi ambao nimewatumikia kwa kipindi hicho hadi sasa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, heshima hii nairejeshwa kwenu kama wawakilishi wa wananchi na pia kwa wananchi wa Bariadi. *(Makofi)*

Ndugu zangu tunaanza mchakato muhimu sana kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia Ibara ya 84 ya Katiba ya Jamhuri

ya Muungano ambayo ni lazima tuisome pamoja na Ibara ya 68. Hatua ambayo tunaanza leo, nasema ni muhimu sana kwa haya yanayofuata ndani ya Bunge hili. Ndiyo maana mnaona *front bench* haipo. Mwakilishi aliyepo wa Serikali humu ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ndiyo msingi wa yeye kuwa humu na atafanya tukio nitakalolisema baadaye.

Baada ya hapo, kama mlivyoona kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge na ratiba yetu, kwa vile yeye ndiye anayeiwakilisha Serikali, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano atakapoleta jina la Mbunge anayempendekeza ashike nafasi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, ni lazima itatolewa hoja ili jina hilo ninyi kama Wabunge mlithibitisha. Hiyo ndiyo kazi nyingine muhimu sana ya msingi.

Hata hivyo, yote hayo hatuwezi kuyafanya mpaka tumpate kiongozi yaani Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama nilivyosema, Ibara ya 84 Ibara ndogo ya kwanza ya Katiba ni lazima tuisome pamoja na Ibara ya 68. Nasema hivyo kwa sababu Ibara ya 68 ndiyo uhalali wa kazi ambayo tunataka kuianza sasa hivi. Ibara hiyo inasema, "Kila Mbunge atatakiwa kuapishwa katika Bunge kiapo cha uaminifu kabla hajaanza kushiriki katika shughuli za Bunge; lakini Mbunge aweza kushiriki katika uchaguzi wa Spika hata kabla hajaapishwa."

Huu ndiyo uhalali wa Kikatiba kwamba ninyi ni Wabunge ambao mnaweza kufanya kazi za Kibunge lakini moja ambalo mnaruhusiwa kulifanya kabla hamjaapa ni hii ya kumchagua Spika wetu. Kwa hiyo, ndiyo tunaanza sasa hatua hii ambayo itatupeleka katika hatua inayofuata. Tukimpata Spika, naye sasa atafanya shughuli muhimu ya kutuapisha kila mmoja wetu. Tukimaliza hapo mambo ndiyo yanaendelea kujipa tena.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nimeona niseme hayo ya utangulizi ili tuweze kwenda vizuri.

Kama nilivyosema nimepewa heshima hii ya kuongoza kikao hiki cha uchaguzi, nianze sasa na hilo la msingi, maana baadhi ya wagombea wetu kwa nafasi ya Spika sio Wabunge, na kwa mujibu wa Kanuni za Bunge ni Wabunge peke yao ndiyo wanaruhusiwa kuingia katika ukumbi huu wa Bunge. Ili hilo sasa liwezekane kufanyika waje waombe kura kwenu, ni lazima waingie ndani. Nawaomba sana tutoe ridhaa hiyo, kwa sababu tusipotoa ridhaa hiyo naamini atabaki mmoja tu na siyo matarajio yetu kwamba iwe hivyo.

Kwa hiyo, naomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali atoe hoja ya kutengua Kanuni ya 143 ili kuruhusu wagombea wa nafasi ya Spika ambao sio Wabunge

waruhusiwe kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge na kushiriki mchakato wa Uchaguzi wa Uspika.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikalii!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA, Ibara ya 84(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 inaweka masharti ya uwepo wa Spika na kwamba atachaguliwa na Wabunge kutoka miongoni mwa watu ambao ni Wabunge au mtu mwenye sifa za kuwa Mbunge;

NA KWA KUWA Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano, linakusudia kumchagua Spika wa Bunge kwa Mujibu wa Kanuni ya 9 ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

NA KWA KUWA, miongoni mwa wagombea wa nafasi ya Uspika siyo Wabunge; na ili washiriki katika uchaguzi huo wanapaswa kuingia Bungeni kwa madhumuni ya kushiriki uchaguzi wa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

NA KWA KUWA, Kanuni ya 143 ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaweka utaratibu maalum kwa Wabunge, Watumishi na Wageni kukaa kwenye ukumbi wa Bunge;

HIVYO BASI, kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1) naomba kutoa hoja ya kutengua Kanuni ya 143 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili kuwaruhusu Wagombea wa nafasi ya Uspika, Dkt. Godfrey Raphael Malisa wa CCK; Dkt. Goodluck Joseph Ole-Medeye wa CHADEMA, Hashim Spunda Rungwe wa CHAUMA, Hassan Kisabi Almas wa NRA, Peter Leonard Sarungi wa AFP, Richard Shadrack Lyimo wa TLP na Robert Alexander Kasinini wa DP ambao sio Wabunge kuingia kwenye ukumbi wa Bunge kushiriki uchaguzi wa Spika wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungani wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana. Tunatengua Kanuni hiyo ya 143. Sasa namwagiza Mpambe wa Bunge aruhusu Wagombea ambao wametajwa na Mheshimiwa

Mwanasheria Mkuu wa Serikali waingie ndani ya Ukumbi wa Bunge. Tunaendelea na hatua inayofuata.

Kwa sababu hili ni zoezi la uchaguzi na Msimamizi wa Uchaguzi wa zoezi hili, yaani *Returning Officer* ni Katibu wa Bunge, nadhani itapendeza kama sasa baada ya hawa Wagombea kuingia, atatoa utaratibu wa uchaguzi wa Spika. Ngoja sasa waingie Wagombea wetu ambao sio Wabunge.

(Hapa Wagombea nafasi ya Spika ambao sio Wabunge waliingia ndani ya Ukumbi wa Bunge)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Hatua inayofuata, Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa maelezo, naomba nitambue uwepo wa Wagombea ili Waheshimiwa Wabunge mfahamu kwamba waliopo ni wangapi. Wagombea wote wapo isipokuwa Mheshimiwa Hashim Spunda Rungwe hayupo katika orodha na wala hatujapokea taarifa ya kujitoa. Kwa hiyo, tunaamini mtaendelea kumpa kura pamoja na yeye kutokuwepo ila hatoweza kujieleza. Lakini akifika wakati zoezi linaendelea, tutaomba Mwenyekiti umruhusu aweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba sasa nitoe maelezo ya uchaguzi.

Kwa wale ambao mnazo Kanuni, maelezo ya Uchaguzi wa Spika yapo kwenye Kanuni ya 9 na Nyongeza ya Kwanza, mnaweza mkafanya rejea. Nitakwenda moja kwa moja katika maeneo yale ambayo tunafikiri mnaweza kuyakumbuka na kuyatumia ili tupunguze muda wa kuzungumza kwa sababu mnazo Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 84 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Spika wa Bunge anachaguliwa na Wabunge kutoka miongoni mwa Wabunge au watu wenye sifa za kuwa Wabunge. Aidha, Katiba inaelekeza kwamba, uchaguzi wa Spika utafanyika wakati wowote katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya na katika Kikao cha Kwanza chochote mara baada ya kutokea nafasi ya Spika kuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti ya Katiba niliyoyaainisha hapo juu, tarehe 28 Oktoba, 2015, niliwaandikia Makatibu Wakuu wa vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu kuwapa taarifa ya awali kuhusu uchaguzi wa Spika na kushauri chama kinachokusudia kusimamisha mgombea katika nafasi ya Uspika kianze mchakato wa ndani. Isitoshe, tarehe 6 Novemba

nilitoa Tangazo la Serikali Namba 514 na kuainisha kwamba kiti cha Spika kitakuwa wazi leo tarehe 17 Novemba kwa mujibu wa Tangazo la Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa barua yangu ya tarehe 9 Novemba, niliviarifu vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu vinavyokusudia kusimamisha mgombea katika uchaguzi huu viwasilishe jina la mgombea huyo kwangu, Msimamizi wa Uchaguzi, tarehe 16 Novemba, saa 10.00 jioni hapa Dodoma, ambayo ndiyo siku ya uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niliwatangazia kuwa chama kinachokusudia kusimamisha mgombea ambaye sio Mbunge kiwasilishe jina la mgombea huyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi, siku tano kabla ya uchaguzi ili Tume ifanye uchambuzi na ikiridhika kuwa mgombea huyo ana sifa zinazotakiwa, Tume itawasilisha jina kwangu siku moja kabla ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokea Taarifa ya Tume ikithibisha kwamba, wagombea wote ambao sio Wabunge walikuwa wana sifa. Hivyo basi, hadi kufikia saa 10.00 jioni siku ya Jumatatu, tarehe 16 Novemba, nilikuwa nimepokea majina ya wagombea nane tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter Leonard Sarungi kutoka Chama cha *Alliance for Tanzania Farmers Party*, Mheshimiwa Hassan Kisabi Almasi wa Chama cha *National Reconstruction Alliance*, Mheshimiwa Dkt. Godfrey Raphael Malisa wa Chama cha Kijamii (CCK), Mheshimiwa Job Yustino Ndugai wa Chama cha Mapinduzi, ambaye ni Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za uchaguzi zinasema, hamruhusiwi kushangilia. Naomba msikilize. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuwe na utulivu. Naelewa hayo yanaashiria nini, lakini Kanuni za Bunge hazituruhusu kushangilia wala kuzomea, lakini zinaruhusu tumezee tu. Kwa hiyo, nitakuwa kidogo mkali na hilo, maana nina mamlaka yote kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tuji-restrain kidogo. Nadhani kiti mnakielewa. Katibu, endelea!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgombea mwingine tuliyepokea uthibitisho wake ni Mheshimiwa Dkt. Godfrey Joseph Ole-Medeye. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Wajumbe, kwa hiyo, mnasawazisha! *Order! Order! Order! (Kicheko)*

Katibu, tuendeleo.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ibaki kwenye record, anatoka Chama cha CHADEMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Richard Shadrack Lyimo - Chama cha *Tanzania Labour Party (TLP)*, Mheshimiwa Hashim Spunda Rungwe - Chama cha CHAUMA na Mheshimiwa Robert Alexander Kasinini - Chama cha *Democratic Party (DP)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagombea wote wamekidhi vigezo na wana sifa za kuwa wagombea wa nafasi ya Uspika.

Waheshimiwa Wabunge, kila mgombea katika hawa nane waliopo atatakiwa kufika mbele yenu kwa kuwa ninyi ndiyo wapiga kura, ili kujieleza, kuulizwa na kujibu maswali, kama yatakuwepo na kuomba kura kwa lugha ya kiswahili au ya kiingereza. Baada ya kujieleza, kila Mbunge atapewa karatasi ya kura yenye majina ya Wagombea wote nane. Tutatoa mfano wa karatasi ya kura na mtaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni karatasi inayofanana na namna hii. Imeandikwa, "karatasi ya kura." Naomba nioneshe japo ni kwa mbali.

(Hapa mfano wa karatasi ya kupigia kura ilioneshwa)

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Jina la kwanza mpaka la nane. Unachotakiwa kufanya ni kuweka alama ya vema kwenye jina la mgombea mmoja tu ambaye unapenda awe Spika. Ukishaweka alama ya "V" moja tu, ukiweka alama mbili karatasi yako imeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kura ni za siri. Baada ya maelezo yote ya wagombea kujieleza, masanduku ya kura yataletwa hapa mbele yakiwa wazi, ili wapiga kura ambao ni ninyi Wabunge muweze kuyathibitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Mbunge ambaye kabla ya shughuli ya uchaguzi kumalizika atakosea katika kuweka alama kwenye karatasi ya kura, ataruhusiwa kumrudishia Katibu karatasi hiyo na papo hapo Katibu ataifuta na kuiharibu na kisha kumpa Mbunge huyo karatasi nyingine ya kura.

Naomba nirejee. Endapo kwa sababu moja au nyingine umeharibu karatasi hii, tunaomba urejeshe ili tukupatie karatasi nyingine, tunahitaji sana kura yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 9(13) mpaka (17), Mgombea atakuwa amechaguliwa kuwa Spika kama atapata zaidi ya nusu ya

kura za Wabunge wote. Iwapo hakutakuwa na mgombea aliyepata zaidi ya nusu ya kura hizo, uchaguzi utarudiwa. Hata hivyo, ni wagombea wawili tu waliopata kura nyingi zaidi kuliko wengine ndiyo watakapigwa kura katika hatua hii ya pili na mshindi atatanzwa kwa kupata kura nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maelezo ya utaratibu wa upigaji kura. Ni matarajio yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mmenisikiliza. Ili twende kwa pamoja, kama kuna tatizo katika uelewa, naomba tuzungumze ili zoezi letu liweze kuwa sahihi. Nina hakika mmetusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maelezo ya Msimamizi wa Uchaguzi. Narudisha kwako ili zoezi la wagombea kujieleza na kuomba kura liweze kufanyika.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Katibu, tunakushukuru kwa maelezo hayo. Kuna Mbunge au Wabunge wanaotaka ufafanuzi? Kama hakuna, nachukulia kwamba maelezo ya Katibu yamejitosheleza. Labda tu mimi niseme moja ambalo lazima tuwe wawazi. Kura zinapigwa wapi? Ni mahali ambapo Mheshimiwa Mbunge, mpiga kura ameketi au watajongea mbele? Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, watapiga kura hapo walipo. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Sasa tumefika hatua muhimu. Kuna mkono! Eeh, Mheshimiwa!

MHE. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa George Mkuchika, Mbunge wa Newala Mjini. Kwa maelezo ya Katibu wa Bunge, suala la maswali halikugusiwa, yatakuwa mangapi? Ni hilo tu.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Kwa Kanuni zetu tulizozoea, kwanza maswali endapo yapo, maana huwezi kulazimisha wapiga kura wakuulize maswali, lakini endapo yatakuwepo, ni maswali yasiyozidi matatu. Kwa hiyo, ndiyo utaratibu ambao tungependa tuende nao.

Ehe, naona mkono, Mheshimiwa Susan Lyimo!

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua utaratibu wa wagombea, je, watakuwa humu ndani wote au watatoka nje, mmoja mmoja aingie?

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Hiyo hatua tunaifikia baada ya haya ya *clarification* kama tumeelewa taratibu.

Mheshimiwa, ili tusaidiane naomba utaje jina.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Mwalimu Marwa Ryoba Chacha, ni Mbunge wa Jimbo la Serengeti. Napenda kujua kabla hatujaendelea, akidi imetimia?

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ni swali zuri. Mwalimu, ni swali zuri sana! Katika hatua hizi ambapo tunataka sasa tuwasikie wagombea, hatuhitaji kujua akidi. Watakapomaliza kujieleza wagombea wetu, sasa hatua hiyo tutaijeleza kwa sababu tunaingia kwa matakwa ya Katiba na Kanuni za Bunge. Kwa sasa hivi umewahisha mambo. Haya, tumalizie jamani maana ni....

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Hapa Mwenyekiti!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Lugola!

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Kangi Lugola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagombea hawa ni wengi na kama ilivyo kawaida ni lazima kiti kitoe maelekezo ni muda gani ambao watautumia kila mmoja kujieleza ili wajue na waweze kujipanga katika kuomba kwao kura na *time keeper* awe *very strict*. Muda ukifika, waambiwe umemaliza, ili sisi tupige kura, tumalize jambo hili. Ahsante.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mimi nadhani tulimalize hapa hapa. Suala la muda ni dakika tatu. Kujieleza ni kuomba kura.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Kuna mkono nyuma! Tutafahamina tu. Bado, aah, Huyu wa kwanza, halafu wewe utakuwa wa mwisho.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Mwalimu Kasuku Bilago wa Jimbo la Buyungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya Spika, ni nafasi nyeti. Hatuwezi kumwelewa Spika tunayemtaka kama atajieleza ndani ya dakika tatu.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tumeshamaliza hilo!

MHE. KASUKU S. BILAGO: Hebu tumwongezee angalau dakika tano ili amwage sera zake hapa. Ahsante.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tumeshalimaliza hilo! Mmeshimiwa Mbunge, tumeshalimaliza hilo. Ehe, Mheshimiwa!

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naitwa Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha. Nauliza kuna wenzetu ambao wana mahitaji maalum, utaratibu uko vipi wa kupiga kura? Ndiyo hilo swali langu.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nakushukuru sana, hilo litaelezwa na Msimamizi wa Uchaguzi, tutakapofikia hatua hiyo.

Mheshimiwa huko nyuma!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naitwa Joseph Mbilinyi, Mbunge Mteule wa Mbeya Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua tu kama uchaguzi huu utakuwa huru na haki, maana *experience* ya uchaguzi uliyopita siyo nzuri sana.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi, sijaelewa ni uchaguzi upi unaoosemea ambao haukuwa huru na haki, lakini mimi nasema hivi, tunaongozwa hapa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni za Bunge. Utaratibu ndiyo huu unaoelezwa. Nimetoa fursa kwa yule ambaye anadhani hajaelewa kinachofuata, ana kiu ya kuelezwa, aelezwe na aelewe, halafu tuingie kwenye shughuli ya Wagombea wetu kujieleza.

Mheshimiwa?

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Ahmed Salum, Mbunge wa Solwa. Nashauri tu tuanze. Nadhani kuhusu *clarification*, kila kitu kimeeleweka. Nashukuru sana. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Sasa tunafikia hatua nyingine muhimu. Tumeshatajiwa majina ya wagombea wetu. Sasa nawaomba wote watoke nje ya ukumbi huu, wataelekezwa mahali ambapo watasubiri na baadaye tutaanza kumwita mmoja baada ya mwingine aje kujieleza hapa hapa.

Wagombea naomba mwelekee kule kwenye chumba ambacho mnapelekwa sasa.

(Hapa wagombea wa nafasi ya Spika walitoka Ukumbini)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Basi, nadhani Mheshimiwa mwenye mahitaji maalum, baki tu wewe ndugu yangu! Mheshimiwa, wewe baki!

UCHAGUZI WA SPIKA

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, sasa tunaanza hatua muhimu ya kuwasikiliza wagombea wetu. Kama tulivyosema, tuna dakika tatu tumetenga kwa kila mmoja. Tunaanza na mgombea tuliyenaye humu ndani, ndugu yetu Mheshimiwa Peter Leonard Sarungi kutoka Chama cha *Alliance for Tanzania Farmers Party (AFP)*.

Ndugu Sarungi, ngoja kwanza. Hawa walio mbele yako ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao ndiyo wapiga kura kwa nafasi ambayo unaiomba. Utapewa dakika tatu kujieleza kwa maana ya kuomba kura. Baada ya hapo, iwapo yatakuwepo maswali utaulizwa maswali yasiyozidi matatu. Karibu na kila la heri.

NDG. PETER L. SARUNGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, wageni waalikwa pamoja na waandishi wa habari *Asalaam Aleykum!*

WABUNGE FULANI: *Waaleykum Salaam!*

NDG. PETER L. SARUNGI: Bwana Yesu Asifiwe!

WABUNGE FULANI: Amen!

NDG. PETER L. SARUNGI: Tumsifu Yesu Kristo!

WABUNGE FULANI: Milele amina!

NDG. PETER L. SARUNGI: Mimi kwa majina, naitwa Peter Leonard Sarungi, ni mwanachama hai kutoka Chama cha Wakulima Tanzania. Nipo mbele yenu kama Mtanzania mzalendo na mwenye nia thabiti ya kulitumikia Taifa hili kupitia nafasi ya Ubunge. Ninayo maono kwa Taifa hili, ninayo maono kwa Bunge hili Tukufu kwa miaka mitano, ninayo shauku ya kufanya yafuatayo katika Bunge; natamani kuliongoza Bunge na kulifanya kuwa ni Bunge moja lenye umoja, huru na lenye kutenda haki bila kujali itikadi na bila kujali makundi.

Niko mbele yenu kusema kwamba natamani kuona Bunge ambalo nitaliongoza lenye kujali maslahi ya Watanzania, maslahi ya wananchi ambao wapo kijijini kule ambao leo wanatusikiliza wakijua kuna Wawakilishi wao humu ndani ambao watawatenda haki.

Nina shauku ya kulifanya Bunge kuondokana na migogoro, Bunge lisilokuwa na migomo, Bunge lisilokuwa na ubabe, Bunge linalotenda haki kwa vitendo. Natamani sana kulifanya Bunge kuwa ni Bunge ambalo litakuwa na heshima maana katika vyombo ambavyo vimebaki vya Serikali vinavyoangaliwa kwa jicho la karibu sana la wananchi ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa hatutaki kuona yaliyofanyika kipindi kilichopita yanafanyika sasa hivi.

Najua kuna changamoto kubwa, lakini nipo tayari kwa maana ya kwamba sitakuwa na makundi humu ndani. Nitakuwa ni Mbunge ambaye nitakuwa naongoza Bunge kwa sheria, kwa taratibu na kanuni ambazo zipo na ambazo tutajiwekea wenyewe. Natamani kuondoa lugha za matusi, natamani kuliongoza Bunge kuondokana na kejeli; natamani kuliongoza Bunge ambalo litakuwa badala ya kujali maslahi ya Watanzania, basi linakuwa linajali maslahi ya vyama; tutarudi kule kule!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana, muda wako umekwisha!

NDG. PETER L. SARUNGI: Waheshimiwa Wabunge, ili kumsaidia Mheshimiwa John Pombe Magufuli, ni lazima tufanye hivyo. Naombeni kura zenu.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ndugu Sarungi!

NDG. PETER L. SARUNGI: Nami natoka kundi maalum, Mkininyima, nimewaletea heshima kubwa sana. Naomba mnipe kura. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Muda umekwisha. Maswali! Mheshimiwa Lusinde!

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Lusinde, Mbunge Mteule wa Mtera. Sielewi kama ni *typing error!* Kwa kuwa Ndugu mgombea ulipoanza, umeanza kwa kuomba nafasi ya Ubunge na sisi humu hatuchagui Mbunge. Sijui kama unaweza kuliweka sawa hilo?

NDG. PETER L. SARUNGI: Sorry, nagombea nafasi ya Uspika. Naomba kura za Spika.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Eeh, swali Mheshimiwa!

(Hapa baadhi ya vipaza sauti vilikuwa havifanyi kazi)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ya jirani yako, mstari mzima, swali limetoweka? (Makofi)

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naitwa Abdallah Mtolea, Mbunge wa Temeke.

Swali langu kwa Mheshimiwa Mgombea ni kwamba najua umekuwa ukifuatilia vikao vya Bunge hili kwa muda mrefu. Je, ni kosa gani ambalo umewahi kulishuhudia likifanywa na kiti cha Spika ambalo wewe tukikupa nafasi ya kuwa Spika hutalirudia? (Makofi)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mh! Mheshimiwa Sarungi!

NDG. PETER L. SARUNGI: Niseme makosa ni mengi, lakini niseme moja tu. Hatujaona kiti kusikiliza kila Mbunge humu ndani na kumtendea haki. Ninaamini mkinipa hiyo nafasi mimi nitakuwa ni Mbunge ambaye nitawasikiliza kila mmoja wenu. (Kicheko)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Eeh, la mwisho!

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naitwa Waitara, Mbunge wa Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Mgombea, sijasikia katika maelezo yako ukitaja elimu yako au uzoefu wa kuongoza chombo chochote kikubwa katika Tanzania ili tupate ushawishi wa namna hiyo. Ahsante.

NDG. PETER L. SARUNGI: Muda ulikuwa ni mchache, lakini niseme kwamba taaluma yangu mimi ni Mhasibu na uzoefu wangu wa uongozi umetokea nilipokuwa kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa IFM. Kupitia vikao mbalimbali nilivyokuwa nikiongoza, viliweza kuleta tija. Lakini baada ya hapo nimekuwa kiongozi wa watu wenye ulemavu katika makundi mbalimbali na ndiyo maana leo nimejitokeza nikiamini kwamba naweza kuwa Mwenyekiti wa Bunge hili. Kuwa Spika. (Kicheko)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Ndugu Sarungi. Haya mpelekeni kule anakostahili kupelekwa.

Waheshimiwa Wabunge, anayefuata ni Mheshimiwa Hassan Kisabi Almasi wa Chama cha *National Reconstruction Alliance (NRA)* aitwe!

(Hapa Mheshimiwa Hassan K. Almasi aliingia Ukumbini)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naona baadhi yetu, *microphone* zetu ziko on. Naomba tuzime, maana zinaingiliana na mawasiliano huku.

Mheshimiwa Hassan Almas karibu. Walio mbele yako ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ndio wapiga kura kwa madhumuni ya nafasi uliyoiomba. umetengewa dakika tatu uweze kujieleza na kuomba kura kwao na baada ya kujieleza, iwapo yatakuwepo maswali, utaulizwa maswali yasiyozidi matatu. Karibu na kila la heri.

NDG. HASSAN K. ALMAS: *Asalaam Aleykum!*

WABUNGE FULANI: *Aleykum Salaam.*

NDG. HASSAN K. ALMAS: Bwana Yesu asifiwe!

WABUNGE FULANI: Amen.

NDG. HASSAN K. ALMAS: Kwa majina naitwa Hassan Kisabi Almasi, Mgombea wa Kiti hiki cha Spika kupitia Chama cha NRA.

Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha leo hapa na kunipa nguvu. Nawashukuru wazazi wangu kwa kunilea vizuri, lakini pia natoa shukrani kwa ndugu zangu wote na pia napenda kuwapongeza Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi. Naamini ninyi ni *cream* ya nchi hii.

Ndugu zangu Wabunge, kilichonivutia kuweza kusimama mbele ya Bunge hili kuomba kura, kwanza kabisa napenda kuliona Bunge hili linakuwa ni Bunge la Kitaifa. Tumezoea kuliona Bunge likiwa ni sehemu ya kufanya siasa ndani ya Bunge kitu ambacho tunaamini Wabunge wenyewe wanatambua kabisa kwamba wanapoingia katika ukumbi wa Bunge wanakuwa ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge ambao wanawawakilisha watu wote wenye vyama na wasiokuwa na vyama katika Majimbo yao. Pia napenda kuona umoja ndani ya Bunge hili na kuweza kuondoa misugvano ambapo watu watajadili maslahi ya nchi hii na kuacha maslahi ya vyama.

Kingine kilichonifurahisha zaidi kabisa ni kuona Wabunge wote walioteuliwa na wananchi kipindi hiki, wengi wao ni Wabunge ambao kweli wana dhamira kabisa ya kuisaidia Tanzania. Nimeona kwa kupitia nafasi hii ya Uspika naweza nikawa Spika mzuri, nikaweza kuwaunganisha Wabunge hawa wakaacha tofauti za vyama nje ya Bunge wakaingia Bungeni kufanya kazi.

Ndugu zangu Wabunge, jambo lingine ambalo nilitaka kusema ni kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano ni muhimili wa tatu wa dola, ni Bunge ambalo linatakiwa liendeshwe bila ushabiki na nimeona kabisa kwamba Bunge hili lazima lipate Spika ambaye atakuwa hana upande wowote ili kuhakikisha maslahi ya wananchi wa Tanzania yanakwenda.

Nimekuwa nikifuatilia Bunge kwa muda mrefu, naona wakati mwingine kunakuwa kuna mambo ya msingi kabisa yanaamuliwa na Spika lakini, kutokana na ushabiki wa vyama Wabunge wamekuwa wakisigana muda wote kana kwamba hilo linalofanywa siyo sahihi. Nina hakika nitafuata taratibu za Bunge, Sheria pamoja na desturi za Bunge.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Almasi muda wako umekwisha.

NDG. HASSAN K. ALMAS: Naombeni kura zenu.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana kwa maelezo yako. Maswali, Mheshimiwa pale!

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jina langu naitwa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Nyag'hwale. Nina swali moja.

Mheshimiwa Mgombea amesema anataka nafasi hii ya Uspika, lakini hajaelezea elimu yake na uzoefu wake. Naomba aeleeze. Ahsante.

NDG. HASSAN K. ALMASI: Nashukuru sana. Kwa bahati nzuri, naweza nikasema mbele ya Watanzania na Bunge hili kwamba uzoefu siyo kitu cha kukiangalia sana. Sababu ni kwamba Wabunge wengi hapa tunategemea wameteuliwa, lakini wamekuja hapa wakiwa sio wazoefu lakini baada ya siku mbili, tatu watakuwa wazoefu; kwa sababu Bunge linaendeshwa kwa taratibu, sheria pamoja na kanuni ambazo lazima kila mtu azifuate.

Kwa hiyo, Kiti cha Uspika kwa sababu tunaamini hakuna chuo kinachofundisha Uspika wa Bunge isipokuwa Mbunge yeyote na mtu yeyote mwenye uwezo anaweza kuwa Spika. Nimeona kabisa kwamba suala la uzoefu haliwezi kuwa ni kigezo kikubwa. Pia kwa sababu ya uzoefu, mimi ni Katibu Mkuu wa Chama cha Siasa, nadhani mnajua kabisa jinsi vyama vya siasa vilivyo na watu makini. Kuwaongoza watu katika chama cha siasa ni kazi kubwa sana. Kwa hiyo, uzoefu kama huo ninao. Elimu yangu ni masuala ya utawala, nimesomea katika Chuo cha Zanzibar, lakini pia nimeweza kusoma kozi mbalimbali ambazo nadhani kwa kupitia nafasi ya Uspika naweza nikawa ni sehemu ya tunda la Taifa hili.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naitwa Msigwa, Mbunge Mteule wa Iringa Mjini.

Ndugu Mgombea, umezungumza jambo moja muhimu sana, umesema uliona kiti kikibeza kwenye mambo ya msingi ya Taifa. Unaweza ukatoa mfano mmojawapo ya kiti kilivyobeza mambo ya msingi ya Taifa halafu wewe utuambie utafanya nini kuachana na tabia mbovu ya kubeza mambo ya msingi wakati Bunge linajadili mambo ya Taifa?

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Kiti gani? Mimi sijabeza hapa! Kiti gani?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Siyo kiti chako, amesema Bunge lililopita.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Hilo siyo swali! (Kicheko)

WABUNGE FULANI: Aaah, swali hilo!

NDG. HASSAN K. ALMAS: Ndugu zangu, namshukuru sana kaka yangu.

Napenda kusema kwamba kama mlinielewa vizuri, nilisema Bunge hili lina taratibu, lina sheria na kanuni zake na desturi za Bunge. Muda wote tunaamini Spika anayesimama mbele ya Bunge hili ni lazima ahakikishe kwamba mwongozo wake ni Katiba, taratibu pamoja na desturi za Bunge. Naweza kusema yafuatayo; nimeshuhudia katika Mabunge yaliyopita, mambo ya msingi yanapoanza kujadiliwa Spika anakuwa ni mtu ambaye anaweza akasimama na kuzuia jambo hilo, katika vikao vya Bunge vingi.

Nadhani haya ndiyo yamepelekea mpaka leo kuona vikao vya Bunge vimekuwa yakizaa vitu vipya kila siku. Kama mnakumbuka, katika vikao vilivyopita tulikuwa tuna kitu kinaitwa G 55 iliyoundwa ndani ya Bunge; iliweza kuvuruga nchi badala ya kuitengeneza. Pia siku hizi mbili zimepita tumeona kuna mengine yamezaliwa katika Bunge, kuna kitu kinaitwa UKAWA nacho kimezaliwa ndani ya Bunge. Ni kwa sababu tu Wabunge wanakuwa siyo kitu kimoja, wanakuwa wana fikra tofauti bila kuwa na fikra moja ya Taifa hili. Kwa hiyo, tunaomba apatikane Spika ambaye anahakikisha kwamba anao uwezo wa kusimamia haya. (Makofi)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Almasi, imetosha, maswali matatu. Tunakushukuru sana. Omba kura Mheshimiwa!

NDG. HASSAN K. ALMAS: Baada ya kusema hayo, ndugu zangu kwa sababu Rais wetu wa Jamhuri amesema tunataka kufanya kazi bila kujali vyama na yuko tayari kufanya kazi na vyama vyote na ninyi Wabunge nadhani mko tayari kufanya kazi na vyama vyote, naombeni kura zenu. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Almasi. *(Makofi)*

Anayefuata! Waheshimiwa naendelea kuwaombeni sana, tujitahidi kujizuia kuonyesha hisia zenu mpo upande gani, kuzomea. Tuko kwenye zoezi la msingi sana la uchaguzi la kupata wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Anayefuata ni Mheshimiwa Dkt. Godfrey Raphael Malisa kutoka Chama cha Kijamii. Aitwe ajongee mbele ya meza.

(Hapa Dkt. Godfrey Raphael Malisa Aliingia Ukumbini)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Malisa karibu Dkt. Godfrey Raphael Malisa, karibu sana. Hawa ndiyo viongozi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ndio wapiga kura kwa nafasi tuliyoimba. Umetengewa dakika tatu kujieleza wewe ni nani; kwa nini unaiomba nafasi hii na mwisho baada ya maelezo yako, iwapo yatakuwepo maswali, utaulizwa maswali yasiyozidi matatu. Kwa hiyo, nakukaribisha, karibu na kila la heri. Anza!

DKT. GODFREY F. MALISA: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni. Naomba kwanza nifanye sahihisho, jina langu kamili ni Godfrey Fataeli Malisa na siyo Raphael, ahsante.

Nichukue nafasi hii kwanza kabisa kwa kifupi ku-*register my disappointment* kutokana na ukweli wa kupewa dakika tatu kwa nafasi ya Uspika, lakini nitajitahidi hizo dakika tatu.

Nawashukuru sana na kuwapongeza Wabunge wote kabisa kwa kuchaguliwa katika Majimbo yenu na ninaamini kabisa mmejipanga vizuri kuleta yale mabadiliko yanayotegemewa.

Pia nawapongeza sana Watanzania wote kwa jinsi ambavyo wameshiriki kuanzia wakati wa kampeni mpaka wakati wa uchaguzi. Napenda kuwashukuru Watanzania wote na ninyi ambao mnawawakilisha. Pia nachukue fursa hii kukushukuru na kumpongeza aliyeapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na kwamba bado kuna wengine wana vidonda, hilo tusilisahau, lakini sasa hivi tuna Rais. Naomba niseme jambo hili halafu nimalizie, naongea dakika tatu. *(Makofi)*

Mimi ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu, nimezaliwa Mkoa wa Kilimanjaro, nimeishi nchini Marekani kwa zaidi ya miaka 15, nikiwa Mwalimu na pia nikiwa mtumishi wa kanisa. Nimegombea Ubunge mwaka ule wa 2010 na mwaka huu pia niliwania nafasi ya Urais kupitia Chama cha CCK, lakini mambo yakaenda ndivyo sivyo. Kwa hiyo, sikuingia kwenye kampeni. Sasa nasimama mbele yenu kuwaomba sana kutoka moyoni nafasi ya kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nathubutu kuomba? Tumemaliza uchaguzi wa kihistoria, uchaguzi wenye *temperature* ya peke yake kabisa na unaanza kuona dalili hata hapa Bungeni, kama tusipopata Spika atakayesimama katikati, Spika asiyetoka huku au kule; na mnanielewa vizuri; sijui tutaendaje kama Taifa! Watanzania wana matumaini makubwa sana.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tuangalie zaidi ya vyama vyetu, tuangalie roho za Watanzania, ndiyo maana wametuamini, wametuweka hapa. Kwa hiyo, naomba mnichague...

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Dkt. Fataeli Malisa!

DKT GODFREY F. MALISA: Nimesikia!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Omba kura.

DKT. GODFREY F. MALISA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge, bila kuangalia wewe ni wa chama gani, najua mambo yanakwenda...

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: He! Tena! Muda umekwisha!

DKT. GODFREY F. MALISA: Naomba kura yako Mheshimiwa Mbunge na Mungu akusaidie unapopiga kura. Amen.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Maswali! Naona moja, Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naitwa Gekul Pauline, ni Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mgombea bila shaka unafahamu majukumu ya Bunge. Unafikiri kwa maoni yako ni jukumu gani ambalo Bunge la Kumi halikutimiza vizuri?

DKT. GODFREY F. MALISA: Swali lako ni zuri sana na ninashukuru kwamba umeniuliza. Mimi sikuwa Mbunge wakati huo, lakini nilikuwa naangalia sana jinsi Bunge linavyoendeshwa. Ni vizuri tuseme huko *site*, yaani huko nje kwa kiasi kikubwa Watanzania wamekuwa *disappointed* na jinsi Bunge la Kumi lilivyoendeshwa. *(Makofi)*

Eeh! Wengine hawatapiga makofi lakini ukweli ni huo kwamba kulikuwa na *issues*. Kwa mfano, mimi niliona *issue* moja kwa macho yangu nikiangalia kwenye TV, *it was very disappointing*.

Ndugu mmoja hapa akataka kupigwa ngumi humu ndani na mmoja akamwita mwenzake tumbili, mwingine sijui kamwita mwenzake nani. Sasa vitu kama hivyo... *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisikii upande huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi Watanzania tumeona na wanatumainia kwamba Bunge hili litakuwa tofauti, litakuwa Bunge ambalo hekima na Burasa vitatawala. Hayo ndiyo matumaini ya Watanzania. Ahsante.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista Mhagama!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kumwuliza swali Mgombea Uspika. Kwa jina naitwa Jenista Mhagama, ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Peramiho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wamemaliza uchaguzi na wamechagua Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama ndiyo Ilani itakayoleta maendeleo ya wananchi katika nchi ya Tanzania katika kipindi cha miaka mitano ijayo; na kazi ya Bunge ni kuhakikisha kwamba Serikali inatekeleza ilani hiyo ya uchaguzi ambayo ndiyo iliyochaguliwa na wananchi katika kipindi husika; swali langu sasa kwa mgombea, je, atafanyaje na atawezaje kusimamia kuhakikisha kama Spika Ilani ya Uchaguzi ambayo imepita inatekelezeka ipasavyo kwa kuzingatia mipango yote itakayoletwa ndani ya Bunge? *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Swali limeeleweka.

DKT. GODFREY F. MALISA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba uniruhusu nijibu swali hilo. Kwanza niseme...

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mimi ndiye Mwenyekiti, jibu.

DKT. GODFREY F. MALISA: Naam!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mimi ndiye Mwenyekiti, jibu.

DKT. GODFREY F. MALISA: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme hivi, Bunge hili likiamua linaweza kuandika historia kwa kumchagua Spika atakayesimama hapa katikati. Hilo la kwanza.

La pili, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge Mteule aliyeliza, pamoja na kwamba Ilani ni ya Chama cha Mapinduzi, lakini ilani ile haileti maendeleo kwa wana-CCM peke yake, inaleta maendeleo kwa Watanzania wote. Kwa hiyo, Spika ana wajibu wa kusimamia taratibu na kanuni zilizopo Bungeni. (Makofi)

Naomba mnisikilize! Spika ana wajibu wa kusimamia kanuni na taratibu na kuishauri au kuibana Serikali ili iweze kutimiza majukumu yake.

Kwa hiyo, kama Chama cha Mapinduzi kwa mfano, kimetoa ilani na mnasema imekubaliwa na wananchi ndiyo maana mkapewa ridhaa ya kuongoza nchi hii, naomba mwelewe kwamba mna jukumu na mna deni kubwa kwa sababu Watanzania wamechoka na ahadi hewa, wanahitaji utekelezaji. (Makofi)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa!

DKT. GODFREY F. MALISA: Samahani, sisemi kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni ilani hewa, sisemi hivyo.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Doctor!

DKT. GODFREY F. MALISA: No! no! Mimi sisemi hilo!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Doctor!

DKT. GODFREY F. MALISA: Ninachosema...

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa tumia *microphone*, una-address the chair.

DKT. GODFREY F. MALISA: Ooh, Okay! Sasa naomba niseme kwamba ilani ya chama chochote cha siasa inapouzwa mbele ya wananchi, haibagui itakadi za wale wanaotendewa kwa mujibu wa ilani ile. CCM au Chama kingine chochote kitakachopata ridhaa kinabanwa na Bunge ili kitimize wajibu wake. (Makofi)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Jenista Mhagama naomba nikuhakikishie, nikisimama hapa kuwa Spika nitaangalia zile taratibu zilizoko katika Bunge na tutawabana Serikali ya Chama cha Mapinduzi pale itakaposhindwa kutimiza ahadi zake na tutaipongeza pale itakapoweza kutimiza ahadi zake. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ahsante sana. Mwishoni huko, la mwisho!

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi naitwa Albert Obama, Mbunge Mteule kutoka Wilaya ya Buhigwe.

Naomba nimwulize *Doctor* hapo, amesema kuna mambo hakuyafurahia kwenye Bunge lililopita, hasa yale ya kuitana tumbili kati ya Wabunge wawili. Mambo yale yalitokea yakiwa yamefanywa na Wabunge na hayakuwa yamefanywa na kiti cha Spika. Je, kwa kuwa haikufanywa na Spika, wewe ungekuwa Spika pale ungechukua hatua gani Wabunge wakijibizana namna ile?

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa, jibu kwa kifupi sana.

DKT. GODFREY F. MALISA: Mheshimiwa Mwenyekiti, okay. Naomba nijibu kwa kusema hivi, ukimpata Spika makini, anayesimamia haki na utaratibu bila kuangalia itikadi za vyama, hayo mambo ya kuitana tumbili humu ndani hayatakuwepo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi kama Spika sitalazimika kuwapatanisha kwa sababu tayari kwa kuzingatia kanuni na taratibu na kuweka maslahi ya wananchi wa Tanzania mbele, hilo halitatokea. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana *Doctor*. Kila la heri. Tumemaliza maswali yako matatu, basi urejee kule kwenye chumba ulipokuwa.

DKT. GODFREY F. MALISA: Naomba kura zote kabisa Waheshimiwa Wabunge bila kujali vyama vyenu. Ahsanteni sana.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ahsante sana. Huyo alikuwa Mgombea wetu wa tatu. Anayefuata wa nne ni Mheshimiwa Job Yustino Ndugai wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge! Waheshimiwa Wabunge!

MBUNGE FULANI: Panya hafundishwi kula usufi. *(Makofi/Vigelegele)*

MBUNGE FULANI: Spika huyoooo!!! Hongera sana! *(Makofi/Vigelegele)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndugai, Mbunge wa Jimbo la Kongwa na Mgomba wa nafasi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, walio mbele yako ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ndiyo unaowaomba kura. Umetengewa dakika tatu kama ilivyo kwa wenzako waliotangulia, ujieleze na uombe kura. Iwapo yatakuwepo maswali, utaulizwa maswali yasisyozidi matatu. Karibu na kila la heri.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, niliyesimama mbele yenu naitwa Job Yustino Ndugai, ni Mbunge wa Kongwa. Mimi ni mwenzenu, ni miongoni mwenu na ni Mbunge mwenzenu. Nimesimama hapa kuomba mnamini kwa kunipa kura ili niweze kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao uzoefu wa kutosha, nayajua matumaini ya Watanzania kwa Bunge la Kumi na Moja na matarajio yao. Ninayo elimu ya kutosha, ninaamini kabisa kwa pamoja tunaweza. Lakini kubwa zaidi, jamani anayekaa na mgonjwa ndiye anayejua amelalaje na ameamkaje! Mimi ndiye niko na ninyi, kwa hiyo ndiye ninayeelewa. Mbunge ukinijia ukiniambia bwana iko hivi, mimi naelewa. Nawaombeni kura zenu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Niangalie wale ambao hawajauliza maswali kabisa! Nakuja, pole pole. Tuanze na Mheshimiwa Mama hapo!

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mgomba kwa nafasi ya Spika, jina langu naitwa Subira Mgalu, ni Mbunge Viti Maalum. Katika Bunge la Kumi, tulishuhudia uwezo wako katika kuisimamia Serikali katika mijadala mbalimbali. Je, kwa nafasi hii unayoomba kwenye Bunge la Kumi na Moja, nini ahadi yako katika dhima kubwa ya nafasi ya Bunge ya kuisimamia Serikali? Ahsante sana.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndugai!

MHE. JOB. Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Subira kwa swali lake zuri. Kama nilivyosema mwanzo, nimekuwa Mbunge katika Bunge hili kwa vipindi vitatu. Nimejifunza mambo mengi chini ya Mzee Msekwa, chini ya Mheshimiwa Sitta na chini ya Mheshimiwa Makinda. Kwa pamoja tumefanya kazi nzuri. Naamini kabisa kwa uwepo wenu na wote ambao tuko humu ndani tuna uwezo kabisa wa

kutekeleza matarajio ya Watanzania. Nawaombeni mniamini, tushirikiane tutekeleze yale tunayotarajiwa kuyafanya. Ahsanteni. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini!

MHE. JOSEPH. R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Mgombea, wagombea wenzako wengi katika kujieleza wamezungumza mambo yanayowahusu Wabunge peke yao, lakini Bunge ni taasisi, lina vyombo vingi, tuko Wabunge, wako wafanyakazi, viko vyombo vya ulinzi na Spika ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi. Pengine ungetueleza ni namna gani kama Spika utasimamia vyombo hivi ili viweze kufanya kazi kwa pamoja kwa maslahi ya Bunge na hasa tukijua kwamba vyombo hivi, kwa mfano, wafanyakazi wa Bunge ndio wanaotusaidia sisi Wabunge kufanya kazi zetu vizuri. Wagombea wenzako hawajazungumza hata kidogo kana kwamba hawapo kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Kwa kifupi Mheshimiwa Ndugai! *(Kicheko/Makofi)*

MHE. JOB. Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Selasini kwa swali lako.

Niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba taasisi ya Bunge naifahamu vizuri na vyombo vyake vyote; Kamati zake zote! Nimeshawahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, nimeshakuwa Mjumbe wa Kamati ya Uongozi kwa miaka sasa, nimekuwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Huduma za Bunge na tumeshughulikia mambo mengi. Niwahakikishie wafanyakazi na sekta zote za Bunge, kwamba kwa uzoefu na elimu ambayo ninayo, wasiwe na wasiwasi. Waheshimiwa Wabunge ninyi wenyewe kama mnavyofahamu, hata ikifika mahali ambapo inabidi tutoke nje tukazungumzie maslahi kwa mfano ya walimu, tutakwenda kufanya hivyo. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nakushukuru. Swali la mwisho, Mheshimiwa Dkt. Tizeba! *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Aaaaah!

MBUNGE FULANI: Ndiyo!

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Charles Tizeba, ni Mbunge Mteule wa Buchosa.

Mheshimiwa Ndugai, tukiacha mambo ya utani kati yangu mimi na wewe nilipenda kujua uzoefu wako wa uongozi huo unaousema, mbona haufanani na

umri wako? Una umri wa miaka mingapi Mheshimiwa kama hutajali?
(Makofi/Kicheko)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa hilo siyo swali. *Gender!* Natafuta *gender balance*. Haya, Mheshimiwa mwenye kufanya hivi, wewe mwenye nguo nyeupe!

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi uliyonipa. Kwa majina naitwa Rhoda Edward Kunchela, ni Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mgombea wa nafasi ya Uspika, nilikuwa nahitaji kukuuliza swali moja. Kwa tathmini ya Bunge lililopita ulionesha ubabe, ulionesha kukibeba Chama Tawala na kuacha matakwa ya wananchi.

Je, umejipangaje kuendeleza ubabe huo endapo ukipewa fursa hii tena?
(Kicheko)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, hilo siyo swali, ni maoni yako. Haitapendeza! Naomba swali, kama hakuna maswali, tum-release Mheshimiwa.

WABUNGE FULANI: Aaah! Huku!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, huku! Huangalii, kushoto!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina Mollel!

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Mollel!

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Hakuna utaratibu hapa!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu!

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naitwa Amina Mollel, ni Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la Kumi lililopita, sisi tuliokuwa nje tulishuhudia baadhi ya Wabunge wakitoka ndani na kususia vikao vya Bunge.
(Makofi)

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilinde!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Endelea tu.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naomba kumwuliza Mgombea Uspika, Mheshimiwa Job Ndugai, ni kwa namna gani ataweza kuhakikisha kwamba Bunge hili, kwa sababu tunapoingia humu ndani tupo kwa ajili ya maslahi ya wananchi... (*Makofi*)

KUHUSU UTARATIBU

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

MHE. HALIMA J. MDEE: Utaratibu! Wafundishe hao manjuka vizuri!

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu. Kuhusu utaratibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba wewe ni mbobezi katika sheria na umekaa humu Bungeni muda mrefu. Bunge linaongozwa na Kanuni, Katiba, sheria na desturi za Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Bunge likishaisha, kwa mfano Bunge la Nane, Bunge la Tisa, Bunge la Kumi; na mambo yake yameisha yanafungwa. Bunge likianza la Kumi na Moja linaanza na mambo yake. Lakini toka maswali yamekuwa yakiulizwa hapa, umekuwa ukiruhusu watu kufanya *reference* ya Bunge la Nane, Bunge la Tisa, Bunge la Kumi. Naomba nikukumbushe Mwanasheria mbobevu kwamba Bunge linaanza na mambo yake, mambo ya Bunge la Tisa yamekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba utaratibu huo uanze kuufuata kuanzia sasa. Kwa hiyo, masuala yote yanayohusiana na Mabunge yaliyopita uyafute tuanze upya.

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Sitaruhusu haya mambo ya utaratibu.

Mheshimiwa Mbunge, anayeongoza kiti ni Mwenyekiti, hakuna mwingine, naomba hili lieleweke. Tupo hapa kwenye shughuli muhimu sana. Nimejaribu sana kufuatilia, maswali mengine nayakataa *outright* kwa sababu ni maoni tu ya mtu. Kuna mengine yanatusaidia kutupatia njia tunapotaka

kwenda kwa nafasi ya Spika. Kwa hiyo, silichukui hilo la Mheshimiwa Zitto Kabwe, lakini nataka tuendelee. Mheshimiwa Ndugai naomba ujibu kwa kifupi tu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Hilo siyo swali.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nasema hivi, ni swali basi!

WABUNGE FULANI: Aaaaah! Sio swali! *(Kelele)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee!

MBUNGE FULANI: Mbona wanazima!

MHE. HALIMA J. MDEE: Siyo swali!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mimi nimempa fursa Mheshimiwa Ndugai kwa kifupi tu.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru sana na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Kama nilivyosema mwanzo, nawahakikishieni ushirikiano wa hali ya juu sana. Ninawahakikishia kutakuwa na Bunge la amani, Bunge la umoja na Bunge la upendo.

Sisi Wabunge wote tutakuwa wamoja kabisa, tutafanya kazi kwa pamoja kabisa kwa malengo yale yale na tutafika salama safari yetu. Nawaomba wote mnipigie kura zenu na mtakapokuwa mnaondoka Dodoma mtaniacha mimi kama mwenyeji wa Dodoma kuwaandalia kila kitu, mnaporudi mnakuta mambo yote safi kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kura zenu! Hapa Kazi Tu!
(Kicheko/Makofi)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Ndugai. Ahsante sana! *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, mgombea anayefuata ni Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Akaribishwe ndani ya ukumbi. *(Makofi)*

(Hapa Mgombea wa nafasi ya Spika Ndg. Goodluck J. Ole-Medeye aliingia Ukumbini)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Haya, imetosha Waheshimiwa!
(Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Dkt. Goodluck Joseph Ole-Medeye, karibu. Hawa waliopo mbele yako ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ndiyo wapiga kura unaoomba ridhaa yao kwa nafasi ya Uspika. Umetengewa siyo zaidi ya dakika tatu kutoa maelezo yako uliyonayo ya kuomba kura. Baada ya hapo, endapo watakuwa na maswali, utaulizwa maswali yasiyozidi matatu. Kwa hiyo, karibu sana, kila la heri.

DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nakushukuru sana na ninamshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amewawezesha Waheshimiwa Wabunge Wateule wote kuwemo humu ndani baada ya kuchaguliwa na wananchi. Nakupongeza sana na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa nafasi hiyo uliyopewa ya kuongoza Mkutano huu na kikao hiki cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa na wananchi na kuwapa dhamana ya kuwawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina kamili ni Goodluck Joseph Ole-Medeye. Wengi hapa wanarifhamu, nilikuwa nanyi katika Bunge la Kumi, hivyo pengine maelezo mengine mengi sitahitaji kuyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakapokuwa Spika wa Bunge hili la Kumi na Moja, ninayo dhima ambayo ninaamini kabisa kwamba tukitekeleza, basi tutaweza kuleta maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kidemokrasia katika nchi hii.

Jambo la kwanza, natambua na ninajua kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge, jukumu kubwa la Bunge hili la kwanza ni kitunga sheria. Sheria zinazotungwa na Bunge hili ndiyo msingi wa utoaji haki katika nchi. Kwa msingi huo basi, kama Bunge litafanya makosa likatunga sheria ambazo zitakuwa na upungufu, zenye mianya ambayo Dola au Mahakama inaweza ikatumia vibaya, basi hakutakuwa na haki katika nchi hii.

Hivyo, lengo langu la kwanza ambalo nitasimamia na litekelezwe nikiwa Spika wa Bunge hili ni kuhakikisha kwamba tunapata Katiba Mpya ili tuweze kuweka misingi ya utoaji haki kwa Watanzania wote, ikiwa ni pamoja na haki za Waheshimiwa Wabunge kushiriki kwa usawa katika mijadala katika Bunge hili.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, natambua wajibu wa Bunge wa kuishauri, kuisimamia na kuiwajibisha Serikali na huo ni wajibu wa Kikatiba. Sasa

ili tuweze kufanya haya, nitashirikiana na Waheshimiwa Wabunge kwa maana ya kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tuketi kama Bunge na tufanye marekebisho makubwa katika mfumo wetu uliopo hivi sasa.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza, nilikuwepo katika Bunge hili kwa miaka mitano. Suala kubwa...

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa *Doctor* omba kura. Muda wa dakika tatu umekwisha.

DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Waheshimiwa Wabunge, nawaomba kura zenu ili niweze kufanya mambo makubwa na marekebisho yatakayowawezesha ninyi Waheshimiwa Wabunge kutekeleza wajibu wenu vizuri ndani ya Bunge na kwenye Majimbo yenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde!

Hivyo, Waheshimiwa Wabunge naomba mnipe fursa. Kauli kwamba usipokuwa Mbunge basi,...

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ole-Medeye omba kura!

DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kura. Ndiyo niko kwenye *process* ya kuomba kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kura kwa Waheshimiwa Wabunge. Nitakapokuwa Spika, nitakuwa Mbunge, hivyo sitakuwa mgeni, sitakuwa nje ya Bunge kama ambavyo wengine wanafikiri hivyo, kwamba kama wewe siyo Mbunge, basi wewe sio sehemu ya Bunge. Kwa mujibu wa Katiba, nitakuwa sehemu ya Bunge na kwa msingi huo nitaweza kusimamia haki zenu ipasavyo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kura zenu wote bila kujali itikadi zenu. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nashukuru, maswali kama yapo!

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa. Naitwa Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mbunge wa Jimbo la Mchinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua Mgombea ni mzoefu Serikalini na ninatambua Watanzania wanaamini kasi ya mabadiliko hivi sasa na wanataka mabadiliko ya kiuchumi ili wapate maendeleo.

Je, Mheshimiwa Mgombea unadhani kwa kasi ya Bunge hili tunahitaji aina gani ya Spika ambaye anaweza kuendana na kasi yetu Wabunge tuliojipanga kwenda kuisimamia Serikali? Nakushukuru.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye!

DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri. Naomba nikiri kwamba nimejaribu kutupa macho kupitia Wabunge wote waliopo hapa, walio wengi ni vijana.

Kwa maana hiyo ni kwamba mtazamo wa Bunge hili ni kesho, siyo jana. Kwa msingi huo basi, tunahitaji Spika mwenye kutazama kesho, sio anayefikiria jana. *(Makofi)*

Hivyo, ninao uhakika kwamba nikipewa fursa hiyo ya kuwa Spika, nina uwezo wa kusimamia Bunge hili ambalo linafanya kazi katika karne ya 21 katika ulimwengu huu wa utandawazi, kwa sababu kama nilivyosema dhima yangu mojawapo ilikuwa ni kurekebisha Bunge ili kuwawezesha Wabunge kuisimamia Serikali, kuishauri na kuiwajibisha inapobidi kwa kushindwa kutekeleza wajibu, kushindwa kutekeleza maamuzi ya Bunge hili pamoja na majukumu mengine iliyokabidhiwa kwa mujibu wa Katiba.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana. Mheshimiwa Nape Nnauye!

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Naitwa Nape Nnauye, ni Mbunge wa Mtama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mgombea, kumbukumbu zinaonesha kwamba uliwahi kutuhumiwa kwa kuwa na tabia ya ubaguzi na tuhuma hizo ziliwahi kutolewa kwenye Bunge la Kumi na Mbunge wa Arusha Mjini, Ndugu Lema. Sasa sijui kama tabia hizo ulishaacha, ili utshawishi kwamba tukikupa nafasi hii hutatumia tabia hizo kuendesha Bunge hili! *(Makofi/Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Siyo swali! Siyo swali!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni tuhuma!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa, hilo siyo swali.

MBUNGE FULANI: Tuhuma ni nyingi, mpaka za madawa ya kulevyala!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Sasa *gender!*

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mbona ulikamatwa na rushwa wewe?

MBUNGE FULANI: Tuhuma, tuhuma!

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mbona umekamatwa na rushwa?

MBUNGE FULANI: ...alipiga ngumi!

MBUNGE FULANI: Hatujibu tuhuma!

MBUNGE FULANI: Bao la mkono!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa hapo!

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Mgombea wa nafasi ya Uspika, ni dhahiri kwamba Watanzania wamekuwa wakitafuta mabadiliko kupitia mfumo wa kidemokrasia kwa maana ya Uchaguzi Mkuu, lakini mabadiliko hayo yamekuwa yakizuiliwa na mifumo ya kizandiki Tanzania Bara na Tanzania Visiwani na kusababisha hali tete mpaka sasa hivi. Je, kama tutakupa ridhaa ya kuwa Spika, umejipangaje kutimiza ndoto ya Watanzania ya kupata mabadiliko kupitia Bunge jipya la Kumi na Moja? Ahsante.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ole-Medeye, sijui ni mabadiliko yapi? (*Kicheko*)

DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake. Napenda kuwahakikishia Watanzania kwamba ni kweli tunahitaji mabadiliko; na tukizungumza mabadiliko katika mazingira ya demokrasia, hayawezi kupatikana kama hatujapata Katiba Mpya itakayotupa Tume Huru ya Uchaguzi, itakayoruhusu kuwepo kwa Mgombea huru pamoja na kufungua milango ya haki kwa Watanzania wote bila kujali rangi, imani wala itikadi. (*Makofi*)

Hivyo, kama nilivyosema katika dhima yangu, hilo ni lengo langu la kwanza kuhakikisha kwamba tunapata Katiba mpya itakayokidhi mahitaji ya Watanzania waliopo leo na watakaokuwepo miaka 200 ijayo. (*Makofi*)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nashukuru. Mheshimiwa Jafo!

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naitwa Selemani Saidi Jafo, ni Mbunge wa Jimbo la Kisarawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua, Watanzania wameridhika na wamekubali *slogan* ya "Hapa Kazi Tu" ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli.

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

MHE. SELEMANI S. JAFO: Katika hilo, nina imani Bunge letu hili sasa, tunapoingia hivi sasa katika Bunge tutaenda na kasi hiyo ambayo Watanzania wameiamini. Je, Mgombea anajipanga vipi kuhakikisha Bunge hili linaenda sawasawa na harakati za Kiserikali za kuhakikisha tunabadilisha maendeleo ya Watanzania? Ahsante. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ole-Medeye!

DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 nilinadi kauli mbiu ya ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi, lakini hatukwenda kwa kasi hiyo wala kwa nguvu hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa kama nikiwa Spika wa Bunge hili, jukumu kubwa la Spika ni kuongoza Bunge hili kama taasisi na kuongoza vikao. Tunachotaka ni Serikali ilete mipango na mapendekezo ya Miswada na Maazimio ambayo italenga kufikia hiyo kauli mbiu ya Mgombea na hivi sasa Rais wa CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ole-Medeye. Maswali matatu yamekwisha. Urejee kwenye sehemu iliyotengwa kwa ajili ya wagombea. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda siyo rafiki na sisi. Mheshimiwa Ole-Medeye, naomba utupishe. Anayefuata ni Mheshimiwa Richard Shadrack Lyimo wa Chama cha *Tanzania Labor Party (TLP)*, naomba aitwe!

(Hapa Mgombea wa nafasi ya Spika Ndg. Richard S. Lyimo aliingia Ukumbini)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Lyimo, karibu. Uliyesimama mbele yao ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ndiyo wapigakura kwa nafasi unayoiomba. Umetengewa kama ilivyo kwa waliokutangulia dakika tatu za kutoa maelezo yako na hatimaye kuomba

kura. Iwapo yatakuwepo maswali, utaulizwa maswali yasiyozidi matatu. Nakukaribisha uanze. Kila la kheri.

NDG. RICHARD S. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Majina yangu naitwa Richard Shadrack Lyimo, ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha *Tanzania Labor Party*. Elimu yangu ni ya Diploma na Uongozi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na hiyo ya Unaibu Katibu Mkuu lakini pia Uenyekiti na nafasi nyingine ambapo muda hauruhusu kuzungumza.

Ndugu zangu, nimeamua kugombea nafasi hii ya Uspika kwa sababu kwanza iko wazi. Nafasi ya Spika iko wazi kwa Mtanzania mwenye uwezo aweze kugombea, ndiyo maana nimeamua. Hilo ni la kwanza.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu!

NDG. RICHARD S. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka niitumie demokrasia kuonesha dunia kwamba ndani ya Bunge hili pengine kunaweza kuwa na demokrasia kuliko wanavyoelewa, kama wataweza kuacha Vyama vyao vyenye Wabunge wakamchagua Lyimo kwa sababu ya uwezo wake wa kuwa Spika wa Bunge, basi nilisaidie Bunge hili kuonesha kwamba Bunge hili lina demokrasia ya kweli.

Waheshimiwa Wabunge, tatu, Bunge ni chombo kikubwa sana na Spika ni mtu muhimu sana ambaye inawezekana kabisa Rais akiwa hayupo wakati mwingine anachukua madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane kwamba dunia na Watanzania wanaliangalia Bunge hili na uendeshwaji wake. Imefikia wakati hata Spika anazomewa. Sasa nimegundua kwamba kuna haja ya kumpata Spika kama Lyimo ambaye ameamua kweli kusimamia haki ndani ya Bunge hili na kuhakikisha kwamba kila Mbunge anaelewa Kanuni na Sheria na ikiwezekana tuongeze uzito wa sheria zitakazombana Mbunge ili Bunge hili liwe na heshima nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kabisa kwamba, tukiangalia mabunge yaliyopita siku za nyuma, yalikuwa na heshima kiasi kwamba Mbunge kwa wananchi alikuwa anaonekana kama ni mtu muhimu sana ndani ya jamii, hata akipita mahali watu wanaogopa. Leo nina wasiwasi, Mbunge wananchi wameshamchukulia Mbunge kama ni mtu wa kawaida kwa sababu ana uwezo wa kuzomea kama wao na wanavizia labda wadai posho. Sasa hili ni lazima lipate Spika ambaye ameamua kuonesha kwamba Watanzania wanataka sasa chombo kitakachojulikana kwa heshima ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba kura zenu na kwamba naweza, nina imani na nina nia. Ni kwamba, mchezaji mzuri wa kufunga magoli ni yule ambaye amekaa nje kwa muda mrefu anaangalia *formation*...

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Omba kura Mheshimiwa.

NDG. RICHARD S. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtakaponichagua mimi, nimeshaona kasoro zipi nitazisimamia vizuri. Tutakuwa na Bunge lenye uwezo na heshima kwa Watanzania.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Omba kura!

NDG. RICHARD S. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, naomba kura zenu zote. Nawapongeza sana kwa kuchaguliwa kwenu na wale waliochaguliwa kwenye Majimbo na kwenye Viti Maalum, naomba kura zenu niwe Spika wenu.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunashukuru. Maswali, kama yapo! Ngoja nione, wale ambao hawajaongea. Wengine wamerudia rudia! Sasa, kule nyuma kabisa! Kule nyuma!

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Maji Marefu.

MBUNGE FULANI: Ni huku Bwana Maji, usiingilie.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mgombea, nashukuru sana kwa hotuba yako nzuri, lakini kuna tatizo moja ambalo umelisema hapa kwamba unataka kutubana Wabunge. Sasa nataka kukuuliza, utakapotubana sisi Wabunge utafanya kazi na nani ndani ya Bunge hili?

NDG. RICHARD S. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa swali lako zuri.

Mimi sitaki nimbane Mbunge wakati anafanya kazi yake vizuri ya Bunge ndani ya vikao na kufuata Kanuni na Sheria zilizowekwa na Bunge lenyewe. Nitaomba Sheria zioneshe pale Mbunge anapotoka nje ya Kanuni. Sheria zilizopo ni nyepesi sana; basi Sheria iweze kutumika kwa Mbunge yule ili kushawishi na mwingine ambaye unataka kufanya kosa kama hilo ambalo linaweza kuathiri heshima ya Bunge asifanye hivyo.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mmh, tunashukuru. Mheshimiwa Kangi Lugola?

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mgombea amejitambulisha kwamba yeye ni Kiongozi Mkuu wa TLP; na kwa kuwa chama hicho kimekuwa kikitakiwa na Msajili wa Vyama vya Siasa kukifuta kwa sababu wamekuwa hawafanyi uchaguzi, hawafanyi chochote kutokana na viongozi hao kuwa mizigo kwenye chama chao, je, haoni kwamba tukimchagua kuwa Spika wetu tutakuwa tumeleta mzigo wa Spika humu ndani, ambaye ameshindwa kuongoza chama, anakimbilia humu Bungeni? (Kicheko)

MBUNGE FULANI: Siyo swali hilo! (Kicheko)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Kangi! Tunaendelea! Gender! Mheshimiwa!

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naitwa Nassari, natokea Arumeru Mashariki.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Aaah! Ngoja bwana! Ngoja, ngoja, ngoja! Mheshimiwa Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naitwa Esther Nicholous Matiko, Mbunge Mteule wa Jimbo la Tarime Mjini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumwuliza ndugu yetu mgombea wa nafasi ya Uspika, katika maelezo yake ameonesha zaidi kwamba akipata nafasi ya Uspika anakuja kuwabana Wabunge. Ningependa aniambie angalau kazi mbili za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ataenda kuhakikisha anazisimamia vipi katika kutekeleza wajibu wake?

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mh! Mheshimiwa Mgombea, kwa kifupi sana.

NDG. RICHARD S. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Tarime Mjini, kwanza hongera sana. Kazi ya kwanza ya Bunge hili ni kutunga sheria. Kwa hiyo, nitasimamia Bunge hili kuhakikisha kwamba linafanya kazi yake vizuri ya kutunga sheria na kuhakikisha zinafanya kazi kama ambavyo zimeelekezwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya pili ni kusimamia utendaji wa shughuli za Serikali. Hili pia nitahakikisha na kwa sababu kuna Kamati nyingi ambazo zitakuwa ni vyanzo vya shughuli mbalimbali za Serikali, nitatoa ushirikiano kwa Kamati hizo kuhakikisha kwamba kila kizuri kilichotokana na Kamati hizo kinafanyiwa kazi na Serikali inashauriwa ipasavyo.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nashukuru, swali la tatu, hili lilikuwa la pili, ngoja nione kule! Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya!

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi ni *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge Mteule wa Jimbo la Nyasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mgombea, ulipokuwa unajieleza, nimekusoma ulikuwa na uchungu sana kuhusu Bunge letu linavyofanya kazi na hasa pale linapofanya mambo ambayo yanalivunjia Bunge heshima na hilo ni jambo muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu. Yawezekana pengine usipate nafasi ya kuwa Spika, lakini hilo jambo linalokuumiza linaweza likachukuliwa na likafanyiwa kazi kwa faida ya nchi. Unaweza ukatuambia ni mambo mangapi, angalau matatu yanayokuumiza sana na kuonesha kwamba Bunge linakosa heshima yake ambayo ulitamani kurekebisha? Unaweza ukatutajia ni mambo gani? Ahsante sana.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Mgombea kwa kifupi sana!

NDG. RICHARD S. LYIMO: Mheshimiwa Manyanya, ahsante sana kwa swali lako zuri. Nikiri mbele ya Bunge hili kwamba nilipokuwa kule Sumbawanga ulinipokea vizuri nikiwa Mjumbe wa Tume, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo nataka nilizungumze ambalo limetokea, nimesema kwamba imefika wakati watu wamesahau heshima ya Spika, sasa wanazomea hata Kiti cha Spika, hilo linauma sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, inawezekana isifurahishe, lakini pia Wabunge tumefikia kuzomea. Tunazomeana sasa Wabunge, jambo ambalo liko mtaani, sasa limerudi Bungeni. Sisemi upande mmoja, pande zote tunazomeana sasa. Wananchi wanashangaa hili ni Bunge gani ambalo limefikia hapo? Hilo linauma sana. Ningepata nafasi, ningetumia nguvu zangu nyingi sana kupambana nalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengine pia ambayo yanafanyika katika Bunge hili, kutoheshimu amri halali ya kiongozi tuliyemweka wenyewe. Kwa mfano, Mwenyekiti hapa anasema tusishangilie, watu wanashangilia vilevile! Sasa tukishafikia hapo, Bunge halitaendesheka. Ndiyo ninachosema mimi! (*Makofi*)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, hayo ni maswali matatu umejibu. Ahsante sana. Urejee kwenye sehemu ambayo

imetengwa kwa ajili ya Wagombea. Ahsante sana. Anayefuata, kwa orodha yetu ni Mheshimiwa Hashimu Spunda Rungwe. Hayupo! Haya.

Waheshimiwa Wabunge, anayefuata ambaye ndiyo wa mwisho, siyo kwa umuhimu, lakini kwa kutajwa katika orodha niliyonayo, ni Mheshimiwa Robert Alexander Kasinini wa Chama cha *Democratic Party (DP)*, aingie ndani ya Ukumbi!

*(Hapa Mgombea wa Uspika Ndg. Robert Alexander Kasinini
aliingia Ukumbini)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Robert Alexander Kasinini, karibu. Walio mbele yako ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ndiyo umekuja mbele yao kuomba kura kwa nafasi ya Spika.

Kama wenzako waliokutangulia, umetengewa dakika tatu za kujieleza na hatimaye kuomba kura. Baada ya maelezo yako, iwapo patakuwepo na maswali, utaulizwa maswali yasiyozidi matatu na hapo itakuwa ndiyo mwisho wa maelezo yako. Kwa hiyo, tunaanza, nakutakia kila la heri. Karibu sana.

NDG. ROBERT A. KISININI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba usahihishe jina langu, naitwa Robert Alexander Kasinini. Mimi ni Mwenyekiti wa *DP* Mkoa wa Iringa na nipo hapa kwa ajili ya kugombea nafasi hii nyeti na muhimu kwa Taifa hili, nafasi ya Uspika wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, nimeamua kuchukua jukumu hili na kitu cha kwanza ambacho nataka nikifanye, nataka nirudishe zile hisia za kweli, imani ya kweli ya wananchi juu ya Bunge hili kwa sababu Bunge lililopita liliua imani ya wananchi juu ya hiki chombo chao kitukufu kinachowawakilisha kwa ajili ya kusimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake katika kutimiza majukumu yake. Kwa hiyo, hilo mkinichagua nitatimiza kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na desturi ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili ndugu zangu, Taifa hili linahitaji watu makini ili waweze kulitoa kutoka hapa lilipo na kwenda mbele zaidi. Uchumi wa dunia hii unakimbia sana, hivyo unahitaji viongozi na vyombo vya Serikali ambavyo vitaiwezesha Serikali na yenyewe kuweza kukimbia kuendana na kasi ya dunia. Tukimpata Spika makini kama mimi Robert Alexander Kasinini tutaweza kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake vizuri, ili tuweze na sisi kukimbia kiuchumi kama ilivyo wale *tiger economy* wa nchi za Asia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, Mabibi na Mabwana, mkinichagua mimi Robert Alexander Kisinini, tutahakikisha kabisa kwamba wananchi wanapata huduma bora za afya, huduma bora za maji ya kunywa na huduma nyingi ambazo wananchi wanastahili kupata ikiwa Bunge hili litaweza kweli kuishauri na kuisimamia Serikali katika kutimiza matakwa yote ya wananchi wangu.

Ndugu zangu, mimi ni kijana mdogo kabisa, nina umri wa miaka 30, mkinipa mimi kiti hiki cha Uspika nina nguvu za kutosha za kutekeleza majukumu yangu ipasavyo. Hivyo ni ninyi tu kuamua, msisite, mumpe Robert Alexander Kisinini ili kweli tuweze kuendana na Bunge lenye viwango na kasi. Ahsanteni sana.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana. Maswali kama yapo! Naona nianze, aah, ni Mheshimiwa nani huyu?

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa majina naitwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Songwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgombea umejieleza vizuri, lakini katika maelezo yako sijakusikia ukizungumzia CV yako hasa katika masuala ya kiuongozi ili basi sisi kama Wabunge tunapochagua tujue tunamchagua Kiongozi wa namna gani.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Kwa kifupi tu Mheshimiwa!

NDG. ROBERT A. KISININI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kwamba muda ambao tumepewa wa dakika tatu hautoshi kueleza kila kitu, lakini kiungozi mimi ni Mwenyekiti wa DP Mkoa wa Iringa na ni mfanyakazi kutoka Shirika la Mama Bahati Foundation ambalo linasimamia masuala ya mikopo na kuwawezesha akina mama Mkoa wa Iringa. Ahsante sana.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nashukuru sana. Kule, Mheshimiwa Ligola!

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ni yeye!

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Naitwa Ali Hassan King, ni Mbunge Mteule wa Jimbo la Jang'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgombea anayeomba Uspika amejieleza hapa kwamba hiyo nafasi inahitaji mtu makini kama yeye ambaye ataweza kufanya kazi vizuri katika Bunge hili.

Sasa nilikuwa namwomba ndugu yangu, angenipa vigezo vitatu vya umakini ambavyo vinahitajika kwa Spika, halafu atutajie na sifa zake yeye tatu za umakini ili tuwe na *confidence* kwamba ataweza kweli kufanya hii kazi. Ahsante sana.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa, kwa kifupi sana, vigezo vitatu. Moja, mbili, tatu. Basi!

NDG. ROBERT A. KISININI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo cha kwanza, mimi ni mcha Mungu, kigezo cha pili, mimi mtu mwenye busara na kigezo cha tatu, mimi mtu mwenye hekima. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Swali la mwisho. Haya, mama! Mheshimiwa, nyuma yako, huyo! Wewe!

MHE. SAUMU H. SAKALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naitwa Saumu Sakala, Mbunge wa Viti Maalum kutokea Pangani.

Mheshimiwa Mgombea, upatapo nafasi hii ya Uspika umejipangaje kuhakikisha watu wenye mahitaji maalum wanapata nafasi sawa hususan kwenye kuchangia? Pia umejipangaje kuhakikisha huendeshi Bunge kwa hasira na jazba tukirejea katika vikao vya Bunge vilivyopita? Ahsante.

NDG. ROBERT A. KISININI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa swali lako zuri. Spika, kama Spika huwa hafanyi kazi kwa kujiamulia, anafanya kazi kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na desturi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, kitu kinachoitwa upendeleo hakipo, isipokuwa tunaangalia sheria zinasemaje? Kanuni zinasemaje? Kwa hiyo, nitaendesha Bunge hili kwa usawa. Hata wale wenye Viti Maalum sidhani kama wana sheria zao tofauti na zilivyo za Bunge hili. Kwa hiyo, nao wanasimamiwa na sheria hizi ambazo mimi nitazisimamia na kuhakikisha kweli zinatekelezeka ili kila mmoja aweze kupata haki yake ya kuweza kushiriki katika Bunge hili. Ahsante sana.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Hapo ndiyo tunafika mwisho wa mahojiano yetu, na wewe Mheshimiwa unaweza ukarejea kule ulikokuwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza sasa moja ya hatua muhimu sana katika zoezi hili. Tumewasikiliza Wagombea wetu walioomba nafasi hii. Kama

tulivyosema, orodha ni wanane, lakini waliofika mbele yenu ni saba. Kwa hiyo, hatua hiyo tumemaliza. Hatua ya msingi ambayo ni ya Kikatiba na Kikanuni ni hii sasa ya kuelekea katika kupiga kura, lakini ili tuweze kufikia matakwa ya Katiba na Kanuni za Bunge letu, naomba sasa nimitake Katibu azingatie utaratibu wa kuwaita Waheshimiwa Wabunge ambao wanawezekana wako nje ya Ukumbi huu waweze kurejea ndani ili hatua zinazofuata tuanze kuzitekeleza. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *Sergeant-At-Arm* piga kengele na Wajumbe popote walipo kwa utashi wao wanaombwa waje ndani kwa ajili ya kupiga kura.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Kuhusu utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa!

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Abdallah Mtolea, Mbunge wa Temeke.

Umesema tulikuwa na Wagombea wanane na saba ndiyo wamepata nafasi ya kujieleza na umesema wote watapigiwa kura wote wanane. Kwa nini tusipate kusomewa japo ile fomu ya huyo mgombea ambaye hajapata nafasi ya kujieleza?

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mimi ni Mwenyekiti wenu. Msimamizi wa Uchaguzi kwa zoezi hili ni Katibu wa Bunge. Maadam Katibu yupo, nitasema yale tu ya utangulizi kwamba tunaongozwa na Kanuni. Kama mpaka tunaingia kwenye zoezi hili msimamizi wa uchaguzi hana taarifa kuhusiana na mwombaji wa nafasi hii ambaye nilitaja jina lake lakini hakuonekana, Mheshimiwa Hashim Spunda Rungwe ambaye anatoka Chama cha CHAUMA. Kwa hiyo, kwa vile katika hatua hii hatuwezi kubadilisha mtiririko wa *ballot paper*, ile karatasi ya kupigia kura, itabidi tufahamu kwamba hali ndiyo hiyo, hakubahatika kufika mbele yetu na wala hatuna taarifa. Kwa hiyo, hali ndiyo hiyo, isipokuwa kama Katibu una ya ziada.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti ni sahihi, isipokuwa kwa kuwa alituthibishia kwamba atafika, tunaomba katika kupiga kura mumpigie kama mtapenda hata kama yeye hayupo. Nilitoa maelezo hayo mwanzo wakati natoa utangulizi. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge ambao ndiyo wapiga kura, katika karatasi ya kura mtakayoiona, jina lake litaendelea kuwepo. Kwa hiyo, tunaomba mkiona inafaa mnaweza kumpigia kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kutoa ufafanuzi mdogo kwamba tuna Mbunge mwenye mahitaji maalum, tumeshaandaa utaratibu wake wa kupiga kura kwa maana ya kuwa na karatasi maalum ya kupigia kura. Lakini pia tumeomba tumpe msaidizi ambaye atamsaidia katika zoezi la kupiga kura.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Katibu. Sasa tufanye zoezi la uhakiki kujiridhisha. Tuko Wabunge wangapi katika ukumbi huu? Swali hili liliulizwa mapema nikasema itafika tu. Sasa ndiyo wakati wake. Kazi hii inafanywa, hivi punde tutawajulisha idadi sahihi ya Wabunge mliopo hapa.

(Hapa Wabunge walihesabiwa)

MWONGOZO WA MWENYEKITI

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mwongozo!

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Miongoni mwa wagombea Ndugu Ndugai ni Mbunge na ni Mjumbe. Kwa bahati mbaya bado yuko nje. Ningependa kujua atahesabiwa huko au ataruhusiwa kuingia ndani wakati wa kupiga kura?

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Nilikuwa naelekea huko. Tulishatengua ile Kanuni ya 143 ya Kanuni zetu kwa wale ambao siyo Wabunge na wenyewe tungependa kwa sababu ya kuonekana siyo kwamba haki itendeke, lakini ionekane kwamba inatendeka kwao kama wagombea, Mheshimiwa Ndugai ni Mbunge ana haki ya kuingia humu bila tatizo, hahitaji kuombewa hiyo idhini maalum. Kwa hiyo, naelekeza wote wakaribishwe warejee ndani, waketi mahali ambapo wataelekezwa ili tunapoanza zoezi hili muhimu na wenyewe wajiridhishe kwamba akidi ipo tunapoendelea sasa kufanya shughuli ya kupata uamuzi. Wakaribishwe, muda siyo rafiki.

(Hapa Wagombea wa nafasi ya Sspika waliingia Ukumbini)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Karibuni tena wagombea. Tunataka na ninyi mshuhudie tukio hili muhimu kama wagombea, lakini ninyi sio Wajumbe isipokuwa mgombea mmoja ambaye ni Mbunge. Kwa maana hiyo, hatua inayofuata, sasa napenda tujiridhishe tuko Wabunge wangapi humu kwa sasa hivi? Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 77(1) akidi ya maamuzi inapaswa iwe ni nusu ya Wabunge wote. Wabunge wote Kikatiba ni 394, lakini Wabunge waliopo kwa

sasa yaani ambao mmesajiliwa ukiacha nafasi za Rais, Baraza la Wawakilishi ni 368. Wabunge mliopo humu ndani kwa sasa ni 359; akidi ni nusu ya idadi ya Wabunge wote ambayo ni 184. Kwa hiyo, tuna akidi ya kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tuendelee na zoezi linalofuata. Naomba kwa ridhaa yako sasa masanduku ya kura yaletwe. Naomba *page girls* na *page boys* na *Sergeant-At-Arms* mlete masanduku ya kura.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Masanduku ya kura yaletwe, tuyaone wote, tujiridhishe kama yamekaa vilivyo. Tulikubaliana tangu mwanzo kwamba zoezi la kupiga kura litafanyika pale pale mahali ulipo, huhitaji kuhangaika. Hatua ya kwanza ndiyo hayo masanduku. Ni yote? Kuna mengine?

Basi, kwa hiyo, naagiza myafungue mwonyeshe kwa wagombea.

(Hapa masanduku yalifunguliwa na kuoneshwa Wagombea na Wapiga kura)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nadhani tumejiridhisha wote. Sawa! Hiyo ni hatua muhimu sana. Hatua inayofuata sasa ni kuletewa karatasi za kupiga kura ili ziweze kugawiwa kwa wenye haki ya kupiga kura. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Tunaomba karatasi za kura zigawiwe kwa Wabunge kwa utaratibu maalum. Tunakwenda kwa *block by block*, yaani upande mmoja baada ya mwingine. Tunagawa upande mmoja, tunamaliza; tunakwenda upande wa pili, tunamaliza.

Kwa hiyo, tunaanza kushoto *block* ya kwanza hii, tunagawa tunakwenda ya pili, tunakwenda ya tatu; na wengine tunakwenda kulia, *block* ya kwanza, ya pili na ya tatu tunakutana katikati. Ambaye atakuwa hajapata karatasi ya kura tunaomba anyooshe mkono au abonyeze *microphone*. Tunaomba Makatibu! *Sergeant-At-Arms*, msimamie ili kuhakikisha kila Mbunge anapewa karatasi moja tu.

(Hapa Wabunge waligawiwa karatasi za kupigia kura)

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, karatasi tunayotoa ya kura tunaomba Waheshimiwa mrejee masahihisho ambayo isingewezekana kuyafanya, lakini tunaomba mtakapokuta jina la Mheshimiwa Dkt. Godfrey Raphael, lisomeke Godfrey Fataeli Malisa na jina la Robert Alexander Kasinini linasomeka Robert Alexander Kisinini. Tunaomba mzingatie hayo wakati wa kupiga kura.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tumepata mistari mingapi imepata karatasi za kupigia kura? Moja, mbili, mh! Wote tumepata karatasi za kupigia kura? Wapi hawajapata? Huko nyuma na mbele hapa! Wangapi hawajapata karatasi ya kupigia kura? Jamani, upande huu!

Waheshimiwa Wabunge, kila mmoja wenu amepata karatasi ya kupigia kura? Ndiyo, nashukuru. Ni hatua muhimu sana! Tutekeleze wajibu! Wenye karatasi ya kupigia kura zingatia maelekezo ya Katibu ili usiharibu karatasi yako ya kupigia kura. Utapigia jina moja tu kwa kuweka alama ya vema mbele ya jina unalolitaka. Ukifanya vinginevyo, kura yako ndiyo imeharibika. Tufanye hilo zoezi sasa hivi ili tukusanye.

Nimepewa hii karatasi ya kupigia kura, kuna Mheshimiwa Mbunge ameingia sasa hivi ambaye hajapiga kura au hajapewa karatasi ya kupigia kura? Tuone mkono wake. Yuko wapi? Hakuna!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Aingie ndani.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Aingie ndani basi tumuone!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Ni yule pale.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Huyo hapo eeh! Sawa sawa! Apewe karatasi yake, haki yake. Waheshimiwa Wabunge mmetekeleza wajibu wenu, sawa!

WABUNGE FULANI: Sawa.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Zikusanywe sasa. Tuko sawa. Tunaweza kuanza kupitisha masanduku Waheshimiwa Wabunge watumbukize. Leta!

Waheshimiwa, tumekusanya kura zote? Bado, bado! Huko nyuma Waheshimiwa hawajatumbukiza kwenye masanduku! Kule nyuma!

Waheshimiwa Wabunge, tayari. Kuna mmoja hapo, wawili na kule nyuma. Wote tumerejesha kwenye masanduku? Sawa.

(Hapa karatasi za kupigia kura zilikusanywa)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Masanduku yote yenye kura zilizopigwa yaletwe mbele yetu hapa. Tayari? Katibu! Katibu yuko wapi?

Waheshimiwa, masanduku yote yako mbele hapa. Sawa!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mimi sina haki ya kupiga kura? Si ndiyo?

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Unayo haki.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Sina! Basi, hii hapa.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Chukua kura ya Mwenyekiti.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda vizuri sana, lakini Waheshimiwa kule nyuma tusikilizane. Ahsante.

Kama kanuni zinavyotaka, Wagombea wetu tunawaomba tuwape fursa ya kila mmoja kuteua mwakilishi wake au wakala kama unataka neno hilo, wa kwenda kusimamia zoezi la kuhesabu kura katika chumba ambacho kimetengwa kwa shughuli hiyo.

Kwa hiyo, tuifanye kazi hiyo na baadaye nitasitisha shughuli hizi kwa muda wa nusu saa halafu kengele itapigwa turejee humu ndani.

Waheshimiwa Wagombea, nitaanza kinyumenyume. Mheshimiwa Robert Alexander Kisinini. Ukipenda mwenyewe unaweza ukasema, mimi nitakwenda mwenyewe, ni haki yako, hiari ya moyo.

NDG. ROBERT A. KISININI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasimamia mwenyewe.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Haya, atakwenda mwenyewe. Mheshimiwa Hashim Spunda Rungwe, anaiamini meza. Mheshimiwa Richard Shadrack Lyimo!

NDG. RICHARD S. LYIMO: Naimanini meza.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Anaiamini meza. Anayefuata ni Mheshimiwa Dkt. Goodluck Joseph Ole-Medeye.

DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, acha nikashuhudie.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ni haki yako. Anayefuata ni Mheshimiwa Job Yustino Ndugai!

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namteua Mheshimiwa Mary Chatanda.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Uje hapa, Mheshimiwa Mary Chatanda ujongee mbele hapa karibu na masanduku. Wagombea na ninyi mje hapa mbele sasa, wenye haki yenu, maana tunataka kuwaona.

Anayefuata ni Mheshimiwa Dkt. Godfrey Fataeli Malisa.

NDG. GODFREY F. MALISA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kuuliza swali. Je, msimamizi nikimteua ni lazima awe Mbunge? Je, ni lazima msimamizi au wakala wangu awe Mbunge? Basi naomba kumteua Mheshimiwa...

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Wakala wako anaweza akawa miongoni mwa Wabunge.

NDG. GODFREY F. MALISA: Siyo nje ya hapo?

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Huwezi kuleta mtu wa nje ya hapo.

NDG. GODFREY F. MALISA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Basi namwomba Mheshimiwa Zuberi Zitto Kabwe. *(Kicheko)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Zuberi Zitto Kabwe, rejea ndani, unahitajika! Unahesabiwa kwa Dkt. Godfrey Malisa. Umeteuliwa! Amekupa heshima kubwa! *(Kicheko)*

Anayefuata, Mheshimiwa Hassan Kisabya Almasi.

NDG. HASSAN K. ALMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana namwomba Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete anisimamie kura zangu. *(Kicheko)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Ridhiwani, umeteuliwa. Nakuomba uje mbele huku. Umepewa heshima kubwa!

Anayefuata ni Peter Leonard Sarungi.

NDG. PETER L. SARUNGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naomba Mwanasheria Mkuu anisadie. *(Kicheko)*

WABUNGE FULANI: Hahaaaaah! *(Kicheko)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ame-decline Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amesema hawezi kufanya hiyo kazi.

NDG. PETER L. SARUNGI: Basi nitasimamia mwenyewe.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Simamia wewe mwenyewe, sawasawa.

Kwa hiyo, mpaka hapo tumekwenda vizuri! Mheshimiwa Ridhiwani kwa heshima, unaweza uka-decline lakini usiketi tu, tunataka Mawakala.

MBUNGE FULANI: Ridhiwani ametoka!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Hayupo! Mbona namwona?

MBUNGE FULANI: Ridhiwani hayupo, amchague Lusinde.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Basi, nadhani shauri ya muda, hebu teua mtu mwingine, au wewe mwenyewe.

MHE. PETER L. SARUNGI: Hapana! Kwa heshima kubwa tu, kwa sababu lengo ni ujenzi wa Taifa. Namwomba Nape Nnauye kama yupo. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Nape hayupo, mchague Lukuvil!

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Sasa naelekeza, wewe mwenyewe uende. Basi ujongee mbele hapo mwongozane sasa kwenda kwenye chumba maalum cha kuhesabu kura. Mtaelekezwa ni wapi. Wafuateni na masanduku ya kura hayo. Sawa!

(Hapa masanduku yenye kura yalipekewa kwenye chumba kwa ajili ya kuhesabu kura)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa hatua hii muhimu tuliyofikia. Kama nilivyosema mapema, nasitisha shughuli ya kikao hiki kwa muda wa nusu saa ili tunyooshe miguu kidogo na baadaye tutarejea ili tupate matokeo ya kazi kubwa mliyoifanya. Ahsanteni. Nadhani tuwe hapa *exactly* saa sita na robo.

(Saa 5.38 asubuhi Bunge lilisitishwa hadi saa 6.15 mchana)

(Saa 6.43 mchana Bunge lilirudia)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kikao chetu kinarejea. Najua kwa mujibu wa Kanuni zetu saa 7.00 ndiyo tunahitaji kusitisha shughuli, lakini kwa sababu ya shughuli tuliyonayo, ni vyema baadaye tutumie Kanuni tuongeze muda wa nusu saa ili tuweze kufanya yale ya msingi kukamilisha zoezi ambalo tulilianza asubuhi. Kwa vile uamuzi huo hauhitaji hoja kutolewa na kuamuliwa, ni mamlaka ya kiti, kwa hiyo, natumia mamlaka niliyonayo kuongeza huo muda wa nusu saa ili tuweze kukamilisha shughuli iliyo mbele yetu. Baada ya kusema hayo, Katibu!

MATOKEO YA UCHAGUZI WA SPIKA

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya zoezi la kuhesabu kura kukamilika, naomba sasa nitoe matokeo.

Idadi ya Wabunge Kikatiba ni 394, idadi ya Wabunge waliosajiliwa na ambao wapo ni 368, idadi ya kura zilizopigwa ni 365, idadi ya kura zilizoharibika ni mbili. Nitasoma matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Godfrey Fataeli Malisa hakupata kura ambayo ni kura sifuri; Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye amepata kura 109; Mheshimiwa Hashim Spunda Rungwe amepata kura sifuri; Mheshimiwa Hassan Kisabi Almas amepata kura sifuri; Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, amepata kura 254; Mheshimiwa Peter Leonard Sarungi amepata kura sifuri; Mheshimiwa Richard Shadrack Lyimo amepata kura sifuri na Mheshimiwa Robert Alexander Kisinini amepata kura sifuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyechaguliwa kuwa Spika ni Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. *(Makofi/Vigelegele)*

WABUNGE FULANI: CCM! CCM! CCM! *(Makofi/Vigelegele)*

MHE. JUMA S. NKAMIA: Wanaisoma namba! Tutawapiga kwa Uspika, CCM mbele kwa mbele! *(Makofi/Vigelegele)*

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mshindi wa Kiti cha Spika amepata asilimia 70 ya kura zote. *(Makofi/Vigelegele)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matokeo ya kazi mliyoifanya. Kwa hiyo, namtangaza mgombea kupitia Chama cha Mapinduzi ambaye ni Mheshimiwa Job Ndugai kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi/Vigelegele)*

Kabla sijamwita ajongee mbele hapa kwa mujibu wa Kanuni, nina tangazo moja ambalo ni muhimu tu nikalisema hapa kwa faida yetu Waheshimiwa Wabunge.

Tangazo hili limetolewa na Mwenyekiti wa muda wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla. Ili kuokoa muda, nilisome tu, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa timu ya Waheshimiwa Wabunge ya *Bunge Sports Club* imeanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Bunge la Afrika Mashariki yatakayofanyika nchini Rwanda mwanzoni mwa mwezi wa 12 mwaka huu.

Kwa kuzingatia hili, Waheshimiwa Wabunge wamechagua uongozi wa muda utakaosimamia maandalizi ya ushiriki wa timu ya Waheshimiwa Wabunge wa Bunge letu. Kwa upande wa mpira wa miguu (*football*), mpira wa pete (*netball*), riadha na mpira wa wavu (*volleyball*) mpaka hapo baadaye uongozi wa kudumu utakapochaguliwa.

Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa ni hawa wafuatao; Mwenyekiti ni Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa William Ngeleja; Mjumbe, Mheshimiwa Ahmed Ngwali na Mjumbe mwingine ni Mheshimiwa Grace Kiwelu. (*Makofi*)

Uongozi wa muda unatoa wito kwa wanamichezo Waheshimiwa Wabunge wahudhurie mazoezi uwanja wa Jamhuri kwa maandalizi ya michezo hiyo. Aidha, imeandaliwa fomu itakayopitishwa kwa ajili ya kujaza mchezo atakaoshiriki Mheshimiwa Mbunge.

Kwa hiyo, nimeona niliseme hili kwa sababu ni faida ya afya zetu na pia kwa sababu ya heshima ya Bunge letu katika michuano inayokuja mwezi Disemba.

Baada ya kusema hayo, kwa sababu tunao wagombea wetu ambao kusema kweli kura hazikutosha, lakini wamesaidia sana katika kuimarisha demokrasia ya kupata uongozi wa Bunge letu, kwa dhati ya moyo wangu nawashukuru sana wote waliojitokeza kupitia vyama mbalimbali ambao tunao hapa. Itapendeza sana iwapo kila mmoja atapewa nafasi hata dakika moja ya kusema neno la shukrani kwa mema ambayo mmewatendea; na hizi ni kura tu, lakini heshima ya Bunge hili na sisi wenyewe kwa niaba ya Watanzania inaendelea kubaki pale pale. Kwa hiyo, mnrufusu tuanze nao kwa mpangilio ambao mtaona ninyi wenyewe inafaa. Labda nianze na rafiki yangu hapa, kwa kifupi tu. Karibu sana!

NDG. PETER L. SARUNGI: Waheshimiwa Wabunge, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi ya kunisikiliza. Vilevile napenda kutoa pongezi

za dhati kwa Mheshimiwa Job Ndugai kwa kushinda kwa kishindo. Mimi kama Peter Sarungi, namwahidi ushirikiano na nipo tayari kuendelea kutoa mashauriano na yeye ili kulifanya Bunge letu kuwa Bunge la mfano kwa Afrika. *(Makofi)*

Vilevile niseme kwamba mmetoa heshima kwa watu wenye ulemavu, nashukuru jambo hili kwa dhati sana kwa maana tumeweza kuonesha kwamba watu wenye ulemavu na wenyewe wanaweza kushiriki katika vyombo vya maamuzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naendelea kutoa rai kwa Serikali Tukufu ya Dkt. John Pombe Magufuli kuendelea kuwakumbuka watu wenye ulemavu na vyama vyote kuendelea kukumbuka watu wenye ulemavu. Tupo watu milioni nne, tunahitaji sauti ya watu wenye ulemavu iweze kusikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Sarungi kwa maneno yako mazuri. Ahsante sana. Mheshimiwa Robert Alexander Kisinini.

NDG. ROBERT A. KISININI: Ahsante sana Ndugu Wabunge wote kwa kutoa ushirikiano pamoja na sisi. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Job Ndugai kwa kuweza kuchukua nafasi hiyo ya Uspika. Sisi tunaondoka tunamwacha yeye. Yesu alipoondoka alisema, mimi naondoka na nawaachieni Roho Mtakatifu.

Sisi tunaondoka, tunawaachieni Job Ndugai akiwa pamoja na Roho Mtakatifu. Tunaamini Bunge hili litakuwa ni Bunge la mfano. Mimi ninawakilisha kundi kubwa la vijana na humu nawaona vijana wengi kabisa ambao wana nyuso za ari ya kazi. Naamini kweli Tanzania itapaa na hatimaye tuwe katika uchumi mkubwa kabisa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana. Namwita sasa Mheshimiwa Richard Shadrack Lyimo.

NDG. RICHARD S. LYIMO: Waheshimiwa Wabunge, kushinda na kushindwa ni sehemu ya mashindano. Kwa hiyo, siyo rahisi sana mtu kufurahia ushindi. Ukiona hivyo, hakuwa mshindani. Lakini kukubali kushindwa pia nayo ni demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kama wangezingatia sana sifa za wagombea tulikuwa tumeshindwa sifa, kwa sababu yule mwenzetu ni mzoefu kidogo. Kwa hiyo, nami nakubaliana na ushindi wake kwamba alistahili kuwa mshindi, wala hakupendelewa, alistahili kwa sifa na heshima aliyonayo

katika Bunge hili kwa muda mrefu. Namwomba tu kwa sababu ametusikia kidogo, basi yale malalamiko tuliyokuwanayo ajaribu kuyafanyia kazi, pengine yanaweza kumsaidia. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Lyimo, tunakushukuru sana kwa maneno yako ya busara. Anayefuata ni Mheshimiwa Hassan Kisabi Almas.

NDG. HASSAN K. ALMAS: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu tumeanza jambo hili vizuri na tumemaliza vizuri. Nataka kusema kwamba ushindi alioupata ndugu yetu Ndugai ni ushindi wa Watanzania, watu milioni 48, kwa sababu Wabunge hawa waliopiga kura hapa wanawawakilisha watu wote katika nchi hii. *(Makofi)*

Jambo la muhimu nililoambiwa kusema ni kwamba naomba sana Wabunge wafanye kazi tumsaidie Rais wetu na tuhakikishe kwamba nchi inafika tunapotaka. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Almas kwa maneno yako mazuri. Sijui kama Mheshimiwa Hashim Spunda Rungwe, ameonekana! Hayupo! Haiwezekani kuwa kwa niaba yake! *(Kicheko)*

Anayefuata ni Godfrey Fataeli Malisa!

DKT. GODFREY F. MALISA. Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa sana Wabunge, nawashukuru kwa mchakato mzima. Pia nachukua nafasi hii kwa dhati kutoka moyoni kumpongeza Mheshimiwa Job Ndugai kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Moja.

Niseme tu neno moja fupi halafu niende nikae. Nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba hatma ya Tanzania ipo mikononi mwenu kabisa! Mtahukumiwa au mtasifiwa kwa jinsi mtakavyowatumikia Watanzania. Namsihi sana Mungu atufungue tusingalie sana vyama vyetu, lakini tuangalie uwezo wa wale watu. Mungu awabariki sana. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Ahsante sana *Doctor* kwa maombi yako na itakuwa hivyo.

Mheshimiwa Dkt. Goodluck Joseph Ole-Medeye! Karibu.

DKT. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nitumie fursa hii ya pekee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kura mlizonipa. Kwa leo hazikutosha, lakini nina imani kwamba

kwa kuwa leo siyo mwisho wa dunia, tutaendelea kurudi hapa na kura siku moja zitatosha. *(Makofi)*

Meshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi leo hii ilikuwa ni sehemu ya kujifunza pia, kwa sababu nimekuwa nikifuatilia uchaguzi huu tokea umeanza kwa mwaka huu; yapo mambo mengi ambayo nimejifunza. Nadhani nitakapokamilisha kitabu changu, mtapata fursa ya kusoma yale ambayo nimejifunza.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kusema kwamba tumempata Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, tumpe ushirikiano ili aweze kutimiza wajibu wake. Lakini labda kwa siku zijazo tungeangalia kuna maeneo ambayo tunahitaji kuyatazama, kwa mfano, tafsiri ya neno "siri" ni nini? Je, kupiga kura kwa makundi kama tulivyopiga leo, kuna siri hapo? Kwa hiyo, labda tungeangalia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie, nilipokuwa hapa kuna Mheshimiwa mmoja aliuliza swali ambalo katika Kanuni tunaita la kuudhi. Naomba nimsamehe kwa sababu pengine bado utoto unamsumbua. Ninaamini atajifunza baadaye. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba kwa namna ya pekee nimpongeze sana Mheshimiwa Job Yustino Ndugai kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Moja. Hongera sana Mheshimiwa Ndugai. *(Makofi)*

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ole-Medeye, ahsante sana. Katibu, hatua inayofuata!

KIAPO CHA UAMINIFU NA KIAPO CHA SPIKA

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Aletwe mhusika, Spika Mteule Job Ndugai! Wahusika wamtafute kokote aliko ili aletwe achukue kiapo.

(Hapa Mheshimiwa Job Y. Ndugai aliingia Ukumbini)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge, ninayo heshima kukuarifu kwamba Wabunge wa Bunge hili Tukufu katika kutekeleza masharti ya Ibara ya 84(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wamekuchagua wewe uwe Spika wa Bunge hili la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo basi, kutokana na kuchaguliwa kwako sasa, nakuita wewe Mheshimiwa Ndugai uape viapo vinavyohusika kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 9(20) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. (Makofi)

KIAPO CHA UAMINIFU NA KIAPO CHA SPIKA

Hapa (Mhe. Job Y. Ndugai) Alipa Kiapo cha Uaminifu na Kiapo cha Spika

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Spika wetu sasa hivi atatoka nje ya ukumbi huu akiongozwa na *Sergeant -At-Arms* (wasaidizi), ili aende akavae rasmi vazi lake. Baada ya hapo atarejea humu ndani kukalia Kiti cha Spika ambayo ndiyo inamaanisha mwisho wa kazi hii ambayo mlinipatia. Ningependa sana niendeleee, lakini kila kitu kina mwisho. Tumeshapata kiongozi wetu. (Kicheko)

Kwa hiyo, nasitisha shughuli ya Kikao chetu kwa muda kuruhusu Spika wetu aende akavae joho na kurejea ndani humu. Ili tuokoe muda, naomba Waheshimiwa tuketi tu humu ndani, kwani haitachukua muda ili nami niweze kujiandaa kutoka vizuri hapa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile tumemaliza zoezi, hawa wageni wetu na wenyewe sasa tuwaruhusu waweze kutoka kabla Spika hajaingia humu ndani. Wanaweza wakapitia huku, isipokuwa huyo rafiki yetu mumsaidie apitie huku.

(Hapa Wagombea wa nafasi ya Spika ambao hawakushinda waliiondoka Ukumbini)

Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alitoka Nje ya Ukumbi na kwenda Kuvaa Joho la Spika

Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Aliingia Ukumbini na Kukalia Kiti

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukiwa tumesimama, naomba sasa tumbe Wimbo wa Taifa.

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama na Kuimba Wimbo wa Taifa)

D U A

Spika (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Naomba tukae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, najua muda hauko upande wetu. Nitatumia dakika chache sana kushukuru, baada ya hapo tufanye kazi kidogo, halafu tutaendelea na utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, natumia nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kura mlizonipa ambazo zimeniwezesha kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Moja la nchi yetu. Kwangu ni historia ambayo haitasahaulika katika maisha yangu. *(Makofi)*

Nilipokuwa mdogo sana, nakumbuka nilikuwa ni mtoto pekee wa mama yangu. Nilikuwa nikimwuliza mama swali moja mara kwa mara kwamba, mama mbona mimi niko peke yangu? Mbona mama fulani ana watoto wengine; na Mama fulani ana watoto wengine? Kwa nini mimi niko peke yangu? Mama nenda zahanati kachukue mtoto mwingine! Wakati huo nilidhania watoto wanapatikana zahanati. Sikumbuki mama alikuwa ananijibu nini? Lakini sikujua kumbe nitakuja kuwa na ndugu wengi sana; na ninyi ndiyo ndugu zangu na Watanzania wengine ambao wako nje ya hapa. Nimepata marafiki, ndugu jamaa wa karibu sana. Nasema ahsante sana kwa Mwenyezi Mungu kwa fursa hii. Ahsante sana kwenu wote. *(Makofi)*

Natambua dhamana mliyonipatia ya kuwa kiongozi wa muhimili huu muhimu sana. Nathamini sana dhamana mliyonipatia. Najua hali ya Watanzania; najua mahitajio yao; najua matarajio yao, naujua umaskini wao; najua nafasi ya chombo hiki katika kuwasaidia Watanzania kutoka hapa walipo; najua kwamba sisi tunapaswa kuwa washauri wazuri wa Serikali ya Awamu ya Tano na ninajua kwamba tunapaswa kuisimamia Serikali ya Awamu ya Tano sisi kama Bunge.

Naomba nitoe wito kwenu Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane wote kwa umoja wetu kama vile Watanzania, kwani wananchi wanatutarajia tushirikiane bila ubaguzi wowote, nami kama Spika nitaongoza katika zoezi hilo la kuhakikisha kwamba hakuna ubaguzi wowote, demokrasia inachukua nafasi, kanuni zinatumiwa na tunajenga upendo na ushirikiano katika Bunge letu. *(Makofi)*

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli ushirikiano wangu binafsi wa Bunge hili na Wabunge wote kwa Serikali ya Awamu ya Tano. Nawashukuru kipekee wananchi wa Kongwa kwa

kuniamini kwa vipindi vinne mfululizo, siyo haba! Baadhi yao wamekuja hapa leo sijui kama wapo, kama watu wa Kongwa bado mpo, naomba msimame pale mlipo. *(Makofi/Vigelegele)*

Ahsanteni sana ndugu zangu, mnipelekee salamu nyumbani. Ahsanteni sana kwa heshima mliyonipa kubwa na heshima ile nitahakikisha nailinda kwa kuhakikisha kwamba siwatii aibu katika Bunge hili.

Mwisho kabisa, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Pius Msekwa ambaye alikuwa Spika wetu kwa malezi na mafunzo; namshukuru sana Mheshimiwa Samuel Sitta kwa malezi na mafunzo; namshukuru sana Mheshimiwa Mama Anna Makinda, ambaye mimi binafsi amenilea hapa Bungeni kwa miaka 15. Alikuwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa miaka mitano; baadaye akawa Naibu Spika, mimi nikawa Mwenyekiti wa Bunge chini yake; baadaye akawa Spika, mimi nikawa Naibu Spika chini yake. Kwa malezi yale na mafunzo ambayo amenipa, namshukuru mama yangu. Naendelea kuwaomba Maspika waliopita wanipe ushirikiano, wasiniache peke yangu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo mafupi, napenda kushukuru tena na kusema ahsanteni sana. Namwomba Mwenyekiti Mungu atutangulie na sisi wote tufuate nyayo ambayo zitaibeba nchi yetu na kuhakikisha kwamba inakwenda mahali bora zaidi kuliko pale mahali ambapo ipo hivi leo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Kiapo cha Uaminifu kwa Wabunge.

KIAPO CHA UAMINIFU KWA WABUNGE

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuvumiliane kidogo tupate kiapo cha Wabunge wachache tu sana, halafu tutaahirisha Bunge hadi jioni ambapo tutaendelea na utaratibu wa viapo tena.

(Waheshimiwa Wabunge Wafuatao Waliapa Kiapo cha Uaminifu)

1. Mhe. George Mcheche Masaju
2. Mhe. Andrew John Chenge
3. Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto
4. Mhe. Richard Mganga Ndassa
5. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu
6. Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu
7. Mhe. Upendo Furaha Peneza

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani sasa mmeona tumeanza kidogo, tutaendelea na zoezi letu leo jioni kwa hiyo naomba muwahi. Kwa jinsi hiyo, naomba nisitishie shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

(Saa 7.34 mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

(Kiapo cha Uaminifu kwa Wabunge kinaendelea)

SPIKA: Kiapo kinaendelea. Nawaomba wale Wabunge ambao majina yao yamekaribia wawe wanajitahidi kuwa karibu inavyowezekana ili tuweze kutumia muda wetu vizuri zaidi, nadhani tumeelewana katika hilo. Kiapo!

8. Mhe. Capt. Abbas Ali Hassan Mwinyi
9. Mhe. Abdallah Ally Mtolea
10. Mhe. Abdallah Haji Ali
11. Mhe. Abdallah Dadi Chikota
12. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru
13. Mhe. Abdallah Hamis Ulega
14. Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood
15. Mhe. Agnes Mathew Marwa
16. Mhe. Balozzi Adadi Mohamed Rajab
17. Mhe. Ahmed Ally Salum
18. Mhe. Ahmed Juma Ngwali
19. Mhe. Aisharose Ndogholi Matembe
20. Mhe. Ajali Rashid Akbar
21. Mhe. Ahmed Makhbut Shabiby
22. Mhe. Aida Joseph Khenan
23. Mhe. Joseph Leonard Haule
24. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi
25. Mhe. Albert Obama Ntabaliba
26. Mhe. Ali Hassan Omar King
27. Mhe. Ali Salim Khamis
28. Mhe. Tundu Antipas Mughwai Lissu
29. Mhe. Allan Joseph Kiula
30. Mhe. Ally Mohamed Keissy
31. Mhe. Ally Saleh Ally
32. Mhe. Amina Nassoro Makilagi
33. Mhe. Amina Saleh Mollel
34. Mhe. Anastazia James Wambura
35. Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest
36. Mhe. Angelina Adam Malembeka

37. Mhe. Angeline Sylvester Lubala Mabula
38. Mhe. Angellah Jasmine Kairuki
39. Mhe. Anna Joram Gidarya
40. Mhe. Anna Richard Lupembe
41. Mhe. Antony Calist Komu
42. Mhe. Antony Peter Mavunde
43. Mhe. Asha Abdullah Juma
44. Mhe. Asha Mshimba Jecha
45. Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji
46. Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye
47. Mhe. Atupele Fredy Mwakibete
48. Mhe. Ally Seif Ungando
49. Mhe. Augustine Vuma Holle
50. Mhe. Augustino Manyanda Masele
51. Mhe. Azza Hillal Hamad
52. Mhe. Bahati Ali Abeid
53. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka
54. Mhe. Saada Mkuya Salum
55. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria
56. Mhe. Boniphace Mwita Getere
57. Mhe. Boniventura Destery Kiswaga
58. Mhe. Catherine Valentine Magige
59. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata
60. Mhe. Cecil David Mwambe
61. Mhe. Cecilia Daniel Paresso
62. Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga
63. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma
64. Mhe. Bernadetha Kasabago Mushashu
65. Mhe. Constantine John Kanyasu
66. Mhe. Dkt. Charles John Tizeba
67. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu
68. Mhe. Dkt. Jumanne Shukuru Kawambwa
69. Mhe. Dkt. David Mathayo David
70. Mhe. Bonnah Moses Kaluwa
71. Mhe. Daimu Iddi Mpakate
72. Mhe. Daniel Edward Mtuka
73. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau
74. Mhe. David Ernest Silinde
75. Mhe. Cosato David Chumi
76. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga
77. Mhe. Desderius John Mipata
78. Mhe. Devotha Mathew Minja
79. Mhe. Almas Athuman Maige
80. Mhe. Balози Dkt. Diodorus Buberwa Kamala

81. Mhe. Doto Mashaka Biteko
82. Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza
83. Mhe. Edward Franz Mwalongo
84. Mhe. Edwin Amandus Ngonyani
85. Mhe. Edwin Mgante Sannda
86. Mhe. Elias John Kwandikwa
87. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu
88. Mhe. Dkt. Elly Marco Macha
89. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka
90. Mhe. Dunstan Luka Kitandula
91. Mhe. Kangi Alphaxard Lugola
92. Mhe. Emmanuel Papian John
93. Mhe. Ester Alexander Mahawe
94. Mhe. Ester Lukago Midimu
95. Mhe. Ezekiel Magolyo Maige
96. Mhe. Faida Mohammed Bakar
97. Mhe. Fakharia Shomar Khamis
98. Mhe. Fatma Hassan Toufiq
99. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile
100. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwanko
101. Mhe. Felister Aloyce Bura
102. Mhe. Flatei Gregory Massay
103. Mhe. Frank George Mwakajoka
104. Mhe. Capt. Mst. George Huruma Mkuchika
105. Mhe. George Malima Lubeleje
106. Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge
107. Mhe. Gibson Blasius Ole-Meiseyeki
108. Mhe. Gimbi Dotto Masaba
109. Mhe. Godfrey William Mgimwa
110. Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel
111. Mhe. Grace Victor Tendega
112. Mhe. Ester Amos Bulaya
113. Mhe. Hadija Salum Ally
114. Mhe. Haji Ameir Haji
115. Mhe. Ester Michael Mmasi
116. Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda
117. Mhe. Haji Khatib Kai
118. Mhe. Halima Ali Mohammed
119. Mhe. Hamad Salim Maalim
120. Mhe. Hamidu Hassan Bobali
121. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa
122. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed
123. Mhe. Mussa Hassan Mussa
124. Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi

125. Mhe. Hussein Mohamed Bashe
126. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali
127. Mhe. Ignas Aloyce Malocha
128. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi
129. Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe
130. Mhe. Jamal Kassim Ali
131. Mhe. Jaffari Sanya Jussa
132. Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga
133. Mhe. Jenista Joakim Mhagama
134. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga
135. Mhe. John Peter Kadutu
136. Mhe. Joram Ismael Hongoli
137. Mhe. Joseph Kizito Mhagama
138. Mhe. Joseph Roman Selasini
139. Mhe. Julius Kalanga Laizer
140. Mhe. Juma Hamad Omar
141. Mhe. Juma Othman Hija
142. Mhe. Jumaa Hamidu Aweso
143. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba
144. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma
145. Mhe. Jesca David Kishoa
146. Mhe. January Yusuf Makamba
147. Mhe. Kemilembe Julius Lwota
148. Mhe. Khalifa Mohammed Issa
149. Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly
150. Mhe. Khalifa Salim Suleiman
151. Mhe. Khamis Ali Vuai
152. Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe
153. Mhe. Khamis Mtumwa Ali
154. Mhe. Khamis Yahaya Machano
155. Mhe. Kiteto Zawadi Konshuma
156. Mhe. Lameck Okambo Airo
157. Mhe. Lucia Michael Mlowe
158. Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma
159. Mhe. Makame Kassim Makame
160. Mhe. Mansoor Shanif Hiran
161. Mhe. Martin Mtonda Msuha
162. Mhe. Mary Deo Muro
163. Mhe. Maryam Salum Msabaha
164. Mhe. Masoud Abdallah Salim
165. Mhe. Kan. Mst. Masoud Ali Khamis
166. Mhe. Mattar Ali Salum
167. Mhe. Maulid Said Abdallah Mtulia

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmetupatia meza katika shughuli hii ya leo.

Kama tulivyoona, orodha yetu ni ndefu lakini baadhi yetu kwa udhuru mbalimbali hawakuwepo, tutajipanga vizuri zaidi ili kusudi kesho tuweze kwenda kwa *speed* zaidi; na mtu hata kama *alphabet* ya jina lako iko nyuma kabisa ni vizuri ukawepo kwa sababu kesho tunaweza tukaanza nyuma tukaja mbele, lakini tutahakikisha kila mmoja anapata fursa ya kuweza kuapishwa.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazie Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwamba kuna kikao cha Wabunge wote wa CCM baada ya kuahirisha Bunge hili kule *White House*.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, sina mengine ya ziada. Kazi za leo zilizopangwa zimekamilika zote. Kwa jinsi hiyo, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.00 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,
Tarehe 18 Novemba, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*